JARIDA KUHUSU |UTALII | UHIFADHI NA MASUALA MBALIMBALI

# TZ&BEYOND

SEPTEMBER 2022 | ISSUE NO 007

Multisectoral magazine



## MATUNDA Ya ROYAL TOUR

HOTELI YA KIFAHARI ZANZIBAR

UWANJA WA NDEGE

UTALII WA BALOON

UTALII BAHARINI

UTALII WA KARAFUU

## WATALII WAONGEZEKA

## MILANGO YA BIASHARAYAFUNGUKA

TSHS. 9,000 KSHS.446 USHS 13,800

5 901234 123457

ISSN 2799-225X | LESENI 00000021

www.tz&beyond.co.tz

Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

# MIFUMO YA HUDUMA BINAFSI KWA **MWANACHAMA NA MWAJIRI**

Mifumo hii ni ya mwajiri **"Employer Portal"** na mwanachama **"Member Portal"** inapatikana kupitia tovuti ya Mfuko **"www.nssf.or.tz"** bofya kifute cha **"Self Service"** (Huduma Binafsi).




- Mfumo wa **"Employer Portal"** ni maalum unaowawezesha waajiri kuangalia michango ya wafanyakazi wao, unaohamasisha uwazi na uwajibikaji kati ya Mfuko na mwajiri.
- Mfumo wa **"Member Portal"** unamuwezesha mwanachama kupata taarifa za michango yake.

@NssfTanzania

# BODI
## YA WAHARIRI


**AFISA MTENDAJI MKUU**

Emmanuel J. Kakuyu
Cell: 0622411148
ekakuyu@gmail.com

**MHARIRI MTENDAJI**

Jimmy C. Kiango
Cell: 0787 180 065
jimmy.kiango@tz&beyond.co.tz

**MSANIFU KURASA**

Felix Jimmy
Cell: 0763 520 319
felix.aloyce@tz&beyond.co.tz

**MWANDISHI**

Hassan Daud
Cell: 0692 695 889

**MWENYEKITI/MLEZI**

Dk. Thomas Kashililah
[fclpp, cipm,ChE, AFA]
Cell: 0754 997 645
namkonda@gmail.com



**TZ&BEYOND**
Mbezi Beach Park Building;
Off Bagamoyo Road
P.O. Box 79010, Postcode: 14121
Phone: +255 655 06 38 39
Dar Es Salaam , Tanzania

**MAUZO/MATANGAZO**
Sales Team,TZ&BEYOND
Cell: 0655063839
email: tz1andbeyond@gmail.com




Royal tour


06 ROYAL TOUR NA MAMBO MUHIMU YA KUKUZA UTALII TANZANIA









83 MATUNDA YA ROYAL TOUR





71 RAIS SAMIA TOUR GUIDE NO. 1’





56 KARIBU ZANZIBAR





83 CNN NAYO YAKUNWA



# Watalii

## KUTOKA KENYA WAONGEZEKA TANZANIA



21 KARIBU TANZANIA



14 JICHO LA TANZANIA



11 THE HIDEN TANZANIA



67 UZURI WA FUKWE ZA ZANZIBAR



57 UTALII WABAHARI



# Royal tour

## NA MAMBO MUHIMU YA KUKUZA UTALII TANZANIA

Safe travels by WORLD TRAVEL & TOURISM COUNCIL





# Royal tour

## JITIHADA NA VIVUTIO VYA UTALII

Pamoja na jitihada za Rais, lakini mdau wa Utalii, John Msengi anasema ipo haja pia ya kuboresha vivutio vya utalii kwa kuongeza mchanganyiko mzuri wa vivutio, **kuanzia kwenye viwanja vya ndege mpaka kwenye maeneo ya utalii.**



NDIO, Rais Samia Suluhu Hassan, ameingia kindaki ndaki kwenye kuutangaza utalii wa Tanzania. Amelifanya hilo kwa yeye mwenyewe kushiriki kwenye kuandaa, kutengeneza na kuzindua filamu ya Royar Tour ambayo wajuzi wa mambo wanasema si jambo rahisi na hata yeye mwenyewe amekiri shuli ilikuwa nzito. Wachambuzi wa masuala ya utalii wameliambia TZ&BEYOND kuwa pamoja na nia hiyo njema ya Rais lakini yapo mambo muhimu ambayo yanapaswa kufanywa na wadau ili kuifanya biashara hiyo kuwa endelevu.

Ikumbukwe kuwa utalii ni biashara kama zilivyobishara nyengine, kanuni na njia zake hazitofautiani na biashara zinazofanyika duniani.

Yapo mambo muhimu ambayo yanapaswa kuzingatiwa katika kuifanya na kuifanikisha biashara hiyo ambayo inatajwa kuingiza fedha nyingi za kigeni nchini.

## KUONDOA CHANGAMOTO

Miongoni mwa mambo yanayopaswa kushughulikiwa ni kuondoa changamoto ya gharama za uendeshaji wa biashara hiyo na kuhakikisha hoteli zinazofikiwa na watalii ni safi na salama wakati wote.




Kuweka mikakati ya kuwajengea uwezo waongozaji watalii na kuhakikisha wote wanatambuliwa rasmi. Kuwapa nafasi wawekezaji wengi zaidi kuwekeza katika sekta ya utalii ikiwemo Hifadhi ya Taifa ya Burigi-Chato.

Changamoto hizi zilishawahi kumkera aliyekuwa Rais wa awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli Julai 9, 2019, alipozindua hifadhi mpya ya Taifa ya Burigi Chato iliyopo Wilaya ya Chato mkoani Geita ambayo ni ya tatu kwa ukubwa baada ya Ruaha na Serengeti.

Alisema pamoja na jitihada zinazofanyika na mafanikio yaliyopatikana, ni wazi kuwa bado mamlaka husika zinahitaji kuongeza bidii zaidi kuvutia watalii wengi ikizingatiwa kuwa Tanzania ina vivutio vingi vya utalii.

## WIZARA IMUUNGE MKONO RAIS SAMIA KWA VITENDO

Ukweli ni kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii, idara na taasisi zake inapaswa kumuunga mkono kwa vitendo Rais Samia kwa kuanza kushughulikia malalamiko yanayotolewa na wadau wa sekta hiyo.

Yapo malalamiko juu ya gharama za utalii nchini kuwa ziko juu na changamoto za usafi kwenye hoteli.

Aidha ipo haja ya kuwajengea uwezo waongaza watalii na kuhakikisha wote wanatambuliwa rasmi ili kutoa huduma bora kwa watalii wanaoingia nchini.

Changamoto kama hii imewekwa wazi pia na mmoja wa wadau wa sekta ya utalii, Leina Lemomo ambaye alisema kuna changamoto kwenye tozo, na ndio maana wameanzisha ushawishi wa tozo maalum za Kiafrika

(African rates) katika maeneo mbalimbali ya utalii.

Leina alisema ndoto zao ni kuona kunakuwa na tozo maalum kwa Waafrika wanapotembelea nchi na maeneo mbalimbali ya bara la Afrika.

“Ndoto yetu ni kuona kunakuwa na tozo maalum kwa ajili ya waafrika tunapotembelea sehemu mbalimbali ndani ya Bara la Afrika, tunataka ukisafiri kiutalii hata kwenye ndege kuwepo na punguzo la malipo maalum kwa waafrika, hivyo hivyo kwenye hoteli mbalimbali barani Afrika.

“Hii inawezekana na inaweza pia kuchochea utalii wa ndani kwa Waafrika. Ukienda mabara mengine tozo kama hizo zipo kwa raia wao na sisi hili kuna haja ya kulipigia debe sote kwa pamoja,” alisema Lemomo.

## KUBORESHA VIVUTIO

Pamoja na jitihada za Rais, lakini mdau wa Utalii, John Msengi anasema ipo haja pia ya kuboresha vivutio vya utalii kwa kuongeza mchanganyiko mzuri wa vivutio, kuanzia kwenye viwanja vya ndege mpaka kwenye maeneo ya utalii.





# THE *Hiden* TANZANIA



# TANZANIA INA JUMLA YA HIFADHI ZA TAIFA 24

ZIMEGAWANYIKA KATIKA KANDA KUU NNE



# THE *Hiden* TANZANIA

Hifadhi za Taifa Kusini mwa Tanzania, jicho lililofumbwa

SASA ni zamu ya The Hiden Tanzania, hii ni awamu ya pili ya filamu ya Royar Tour, ambayo kimsingi imekuwa na mafanikio makubwa.
Rais Samia Suluhu Hassan, ndie mshiriki mkuu wa The Hiden Tanzania na ameahidi kulifanya hili kwa ukamilifu.

Pengine utajiuliza The Hiden Tanzania ni nini? Hii ni mwendelezo wa filamu ya Royar Tour.

Lakini The Hiden Tanzania itaangazia zaidi vivutio vya utalii ambavyo si maarufu/

Tayari Rais Samia amesema kuwa serikali imeshakamilisha mchakato wa filamu hiyo na miongoni mwa vivutio vitakayonufaika ni vile vilivyopo kwenye mikoa ya Nyanza za juu kusini.

Aliyasema hayo alipozungumza na wakazi wa mkoa wa Njombe, ujio wa filamu hiyo ni mwendelezo wa kuutangaza utalii wa Tanzania.


Royal tour
Jicho
LA
TANZANIA

Idadi kubwa ya wadau wa sekta ya utalii nchini wanaamini eneo pekee lenye vivutio vya utalii Tanzania ni ukanda wa Kaskazini unaojumuisha mikoa ya Tanga, Arusha Manyara na Kilimanjaro.

Hata baadhi ya viongozi huamini kuwa suala la utalii nchini linabebwa na mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara, huku mikoa mingine ikijikongoja tu, fikra ambazo hazibebi uhalisia.

Ukweli ni kwamba Tanzania imebarikiwa kuwa na vivutio vingi vya utalii katika maeneo mengi na ni miongoni mwa nchi chache barani Afrika zinazotembelewa na watalii wakati wote wa mwaka.





Maeneo yanayovutia utalii ni wanyamapori ambao wanapatikana kwenye hifadhi za Taifa na kwenye mapori ya akiba.

Kwa sasa Tanzania ina jumla ya hifadhi za taifa 22 zilizogawanyika katika kanda kuu nne ambazo ni Kanda ya Kusini ambako kunapatikana hifadhi ya taifa Ruaha na Milima ya Udzungwa, Kaskazini inapatikana hifadhi ya taifa Ziwa Manyara na Tarangire, Magharibi inapatikana hifadhi ya taifa ya Katavi na Milima ya Mahale na kwa kanda ya Mashariki ipo moja tu ambayo ni hifadhi ya taifa ya Saadani.

Ukanda huu wa kusini hifadhi zake zinapatikana Kusini mwa Tanzania ambazo ni hifadhi ya taifa ya Ruaha, Mikumi, Milima ya Udzungwa na hifadhi mpya ya Mwalimu Nyerere (ambayo hapo zamani ilijulikana kama pori la akiba la Selous).

## RUAHA

Awali hifadhi ya Taifa ya Ruaha ilikuwa ni pori la akiba la saba kabla ya kupewa hadhi ya kuwa hifadhi ya taifa mwaka 1964.

Mkoa wa Iringa ndio umetoa eneo kubwa la hifadhi hiyo yenye utajiri mkubwa wa wanyamapori ukifuatiwa na mkoa wa Mbeya.



Takwimu za utafiti wa makazi na idadi ya tembo uliofanyika mwaka 2014 zilibainisha kuwa 'Rungwa-Ruaha ecosystem' ndiyo yenye makundi makubwa na idadi kubwa ya tembo nchini.

Aidha hifadhi ya taifa ya Ruaha imetajwa kuwa na Simba ambao ni saw ana asilimia 10 ya Simba wote waliopo duniani.

Kwa upande mwengine hifadhi hiyo inatajwa kuwa na idadi kubwa ya wanyama wanaokula nyama kama Chui, Duma, Fisi na Mbwa mwitu.





Hifadhi hiyo pia ni maarufu kwa kuwa na idadi kubwa ya tandala wakubwa na wadogo pamoja na na miti ya mibuyu yenye umri mkubwa.

## MILIMA YA UDZUNGWA

Mwaka 1992, Serikali ya awamu ya pili ililipa hadhi eneo hili kuwa hifadhi ya taifa kutoka kwenye hifadhi tano za misitu.

Milima ya Udzungwa inapatikana Morogoro na milima hii inaingia kwenye safu za milima ya Tao la Mashariki (eastern arc mountains) yenye utajiri mkubwa wa aina mbali mbali za viumbe pori.



Misitu hii inasadikiwa kuwa na miaka milioni 30 na inaelezwa kuwa ilikuwa imeungana na msitu wa Congo (congo basin) na Afrika magharibi lakini kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi na shughuli nyingine za kibinadamu ikapungua na kubakia sehemu chache chache.

## MIKUMI

Kabla ya pori la akiba la Selous halijaingizwa kwenye hifadhi ya taifa ya Mwalimu Nyerere, Hifadhi ya taifa ya Mikumi ilikuwa ikishika nafasi ya nne kwa ukubwa Tanzania.

Eneo hili liliteuliwa na kuwa hifadhi ya taifa mwaka 1964 ikiwa na jumla la kilomita za mraba 3230.







Hifadhi ya taifa ya Mikumi ni miongoni mwa hifadhi iliyopitiwa na barabara kuu ya Tanzania-Zambia, ikiwa inapakana na Selous upande wake wa Kusini, Hifadhi ya milima ya Udzungwa na milima ya Uluguru.

Hifadhi hii inasadikiwa kuendana na tambarare ya hifadhi ya taifa ya Serengeti na ni rahisi kuona Simba wanaopanda miti mikubwa tofauti na wale wa hifadhi ya taifa ya ziwa Manyara.



## MWALIMU NYERERE

Sehemu kubwa ya hifadhi hii ya taifa ya Mwalimu Nyerere, lilikuwa ni pori la akiba la Selous.

Mwaka 1922 eneo hili lilianzishwa kama Pori la Akiba na mapema mwaka 2019 liliteuliwa na kuwa hifadhi ya taifa ya Nyerere ikiwa na ukubwa kilomita za mraba 50,000 hivyo kuwa hifadhi ya kwanza kwa ukubwa Afrika Mashariki.

Mwaka 1982, UNESCO ililitenga eneo hili kama urithi wa dunia (world heritage site) kutokana na uwepo wa wanyama wengi tofauti tofauti na pia kuwa eneo ambalo halijaharibiwa.



Wanyama wanaopatikana kwenye hifadhi hiyo ni Tembo wa msituni, Faru weusi, Mbwa Mwitu, Twiga, Pundamilia na Mamba.

Ipo dhana kuwa uwapo wa shughuli ya uchimbaji wa bwawa la umeme na hadi kukamilika kwake mwaka 2022 kunaweza kulipotezea hadhi ya kuwa eneo la urithi wa dunia.

## MBONI ILIYOFIFIA

Ukanda wa hifadhi za taifa za Kusini, una vivutio vingi vya utalii ukiachana na wanyamapori waliopo kwenye hifadhi za taifa pia kuna wanyamapori waliopo kwenye mapori ya akiba mfano Mpanga-Kipengele, misitu ya asili na yenye historia za makabila kama msitu wa Nyumba nitu







mkoani Njombe, vivutio vya kihistoria kama bonde la Isimila, Kalenga kwenye fuvu la Chifu Mkwawa, majengo ya wakoloni ambayo yametawanyika sana mjini Iringa na baadhi ya sehemu za mkoa wa Njombe na Mbeya, daraja la ajabu maarufu kama Daraja la Mungu lililopo mkoa wa Mbeya, maji moto na ziwa Nyasa ambalo hutumika kama mpaka wa Tanzania na Malawi.

# CHANGAMOTO

## HIFADHI YA TAIFA KANDA YA KUSINI









Kanda hii imekuwa ikipokea watalii wachache sana ukilinganisha na hifadhi za taifa zinazopatikana ukanda wa Kaskazini ambazo ni hifadhi ya taifa ya Serengeti, Arusha, Tarangire, Mlima Kilimanjaro, Ziwa Manyara na Mamlaka ya hifadhi ya eneo la Ngorongoro.

Uchache huu wa watalii umesababishwa na umbali wa kutoka kwenye miji hadi hifadhini, lakini pia kukosekana kwa viwanja vya ndege vyenye uwezo wa kupokea ndege kubwa, hatua inayosababisha umbali mrefu kutoka Dar es Salaam hadi ziliko hifadhi hizo.

Miundo mbinu bado ni duni, kuifikia hifadhi ya taifa ya Ruaha kutoka Iringa mjini ni mwendo wa saa mbili huku barabara iliyopo ni ya vumbi.

Ukanda wa Kusini kwa ujumla wake bado hauna mwamko wa utalii hali inayochangiwa na kutotangazwa kwa vivutio vilivyopo.

Kukosekana kwa matangazo ya kutosha juu ya hifadhi za kusini, kunazichelewesha kujulikana kimataifa na hasa ikizingatiwa kuwa hifadhi nyingi za ukanda huo zilianzishwa mara baada ya nchi Tanganyika na baadae Tanzania kupata uhuru, tofauti na zile za ukanda wa kaskazini ambazo zilikuwepo hata wakati wa ukoloni.

Mathalani hifadhi ya taifa ya Serengeti ilianzishwa mwaka 1959 chini ya utawala wa kikoloni, hii inamaanisha hifadhi hiyo imepata nafasi ya kutangazwa na wao wenyewe.

## NINI KIFANYIKE?

Zipo njia zinazoweza kutumiwa ili kufumbua jicho hili lililofumbwa kwa sababu kadha wa kadha.

Kuboresha na kuimarisha miundo mbinu karibu na hifadhi hizi na ndani ya hifadhi zenyewe. Kujenga barabara za lami.

Kujenga na kuboresha viwanja vya ndege vilivyopo kwenye mikoa inayohodhi hifadhi hizi.

Kutangaza, kufufua, kuboresha na kuimarisha vivutio vyote vya kihistoria na asilia vinavyopatikana ukanda wa kusini, hatua hii itasaidia kuongeza vivutio vingi Zaidi. Wizara na idara zinazohusika na sekta ya utalii zinaweza kuboresha vivutio vya utalii kwenye barabara ya kutoka Mikumi hadi Ruaha.

Inaweza kuboresha na kuimarisha barabara za kufikia Isimila kwenye mabaki ya mawe yaliyotumiwa na watu wa kale (kipindi cha zama za mawe), Kalenga kwenye historia ya Chifu Mkwawa wa kabila la Wahehe na majengo yenye historia hasa kwa kipindi cha vita ya Mkwawa na Wajerumani yaliyopo Iringa mjini.

Maeneo yote haya yanaweza kuwa chachu ya utalii kwa ukanda wa Kusini.

Kuandaa maonyesho mbalimbali yanayohusu tamaduni nyingi za watu wa Kusini yanayohusisha ngoma, ufumaji, ususi, mavazi, vyakula, na historia ya kila kabila.

Kuwa na mahali rasmi panapoweza kubeba historia za makabila ya ukanda huo, kama ilivyo kwa Kijiji cha Makumbusho, kilichopo jijini Dar es Salaam.

Kubuni bidhaa inayouzika sana dunia inayozalishwa zaidi ukanda wa kusini mwa Tanzania na kuipa jina mojawapo la hifadhi za ukanda huu.

Gharama za uwekezaji kwenye sekta ya utalii hasa kwa ukanda wa Kusini zipunguzwe ili kuvutia wawekezaji wengi Zaidi kwenye eneo hilo.

Elimu ya utalii itolewe zaidi kwa watanzania hasa waishio kwenye ukanda huo wa kusini ili kujua umuhimu wa kutembelea vivutio vyao.




Royal tour
Karibu
Tanzania



# Hifadhi za Taifa Tanzania

ZILIANZISHWA KWA MUJIBU WA SHERIA YA HIFADHI ZA TAIFA TANGANYIKA SURA YA (412) YA MWAKA 1959 KWA AJILI YA KUHIFADHI MIFUMO YA EKOLOJIA KATIKA MAENEO YOTE YALIYOTENGWA









TANZANIA KWA SASA NDIO INAONGOZA NCHI ZA AFRIKA KWA KUWA NA IDADI KUBWA YA HIFADHI ZA TAIFA, AMBAZO ZIMEFIKIA

24




# Karibu Tanzania

10 SEPTEMBA 2019, BUNGE LA TANZANIA LILIKUBALI KUUNDA MBUGA TATU ZA TAIFA NA KUFANYA IDADI YA MBUGA NCHINI KUFIKIA 24

Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) zilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Hifadhi za Taifa Tanganyika Sura ya (412) ya mwaka 1959 kwa ajili ya kuhifadhi mifumo ya ekolojia katika maeneo yote yaliyotengwa kama hifadhi za Taifa pamoja na kupanua hifadhi zilizopo.

Utalii wa wanyama pori na mimea ni chanzo kukuu cha mapato yanayorudishwa kugharamia usimamizi, udhibiti, urekebishaji na utimizaji wa majukumu yote ya kiuendeshaji ndani ya hifadhi. Tanzania kwa sasa ndio inaongoza nchi za Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya Hifadhi za Taifa, ambazo zimefikia 24.

Septemba 10, 2019, Bunge la Tanzania lilikubali kuunda mbuga tatu za Taifa na kufanya idadi ya mbuga nchini kufikia 24 ambayo ni idadi ya juu zaidi barani Afrika.



Kwa kuzingatia nia njema ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuutangaza utalii kimataifa ili kuvutia watalii na wawekezaji, jarida la TZ&BEYOND limeiona haja ya kuzibainisha baadhi ya hifadhi za Taifa zilizopo nchini ambazo zinavutia na mtalii anaweza kutembelea wakati wowote ndani ya mwaka.

Mbali na kuziainisha, lakini pia jarida hili litafafanua kwa kina aina ya vivutio vilivyopo kwenye hifadhi hizo na namna ya kufika.



# Hifadhi ya Saadani











Hifadhi ya Taifa ya Saadani ipo katikakati ya pembe tatu ya historia ya Bagamoyo, Pangani na Zanzibar.

Hifadhi hii ina eneo la kilomita za mraba 1,100, ni hifadhi pekee ya wanyama Tanzania inayopakana na bahari.

Tabia ya nchi ni ya mwambao, joto na unyevunyevu, ina mchanganyiko wa kipekee wa mimea na wanyama wa baharini na nchi kavu katika eneo lenye utamaduni wa kustaajabisha.

Kuna takribani spishi 30 za mamalia wakubwa pamoja na aina mbalimbali za watambaazi na ndege.

Licha ya spishi nyingi na samaki (zaidi ya 40), Kasa wa Kijani, Nyangumi wenye nundu na Pomboo wanapatikana pia katika eneo la karibu na bahari.

## NAMNA YA KUFIKA

Kwa barabara, Hifadhi ya Saadani ipo kiasi cha kilomita 45 Kaskazini ya Bagamoyo.

Hifadhi hiyo itafikiwa kwa urahisi zaidi kupitia Mto Wami kutoka Dar-es-salaam kupitia Bagamoyo mara baada ya daraja linalojengwa hivi sasa litakapokamilika.

Hata hivyo, hivi sasa kufika kwenye hifadhi kutoka Dar-es-salaam ni lazima uzunguke kilomita 200 kupitia barabara ya Chalinze-Msata. Kutoka upande wa Kaskazini, mtu anaweza kufika kwenye hifadhi kutoka jiji la Tanga kwa kuvuka Mto Pangani kwa feri (umbali wa kilomita 75/ mwendo wa saa tatu kwa gari).

Zanzibar iko umbali wa kilomita 40 kutoka kwenye hifadhi. Kuna usafiri wa kila siku kwa basi kutoka Dar-es-salaam na kijiji cha Saadani pamoja na Tanga na kijiji cha Mkwaja.

Kwa ndege, usafiri wa ndege unaweza kuandaliwa kwenda kiwanja kidogo cha ndege cha Mkwaja au Saadani.

## MAJIRA

Majira ya mvua (Machi-Aprili) barabara za tope zinaweza kufanya usafiri katika upande wa kusini mwa hifadhi kuwa mgumu hivyo mtalii anashauriwa kujua hali ya barabara kabla ya kusafiri.

## CHAKULA NA MALAZI

Nyumba za wageni za TANAPA na vibanda vinapatikana katika Kijiji cha Saadani na Makao Makuu ya Hifadhi, Mkwaja.

Kuna maeneo mengi ya kupiga mahema kwenye hifadhi kama vile mwambao wa mto Wami(Kinyonga), Tengwe na maeneo ya kupiga mahema ya ufukoni.

Kuna maeneo mengine ya malazi na chakula ya binafsi ndani na nje ya hifadhi kama vile Saadani Safari Lodge , Kisampa na mahema yanayotoa nafasi ya kuangalia mandhari ya hifadhi.

HIFADHI HII INA ENEO LA KILOMITA ZA MRABA

**1,100**

NI HIFADHI PEKEE YA WANYAMA TANZANIA INAYOPAKANA NA BAHARI.

# Hifadhi ya Katavi



HIFADHI HII NI YA TATU KWA UKUBWA TANZANIA KWA KUWA NA ENEO LA KILOMITA ZA MRABA

4471




## HIFADHI YA TAIFA KATAVI

Hifadhi ya Taifa ya Katavi iko wilaya ya Mpanda magharibi mwa Tanzania. Hifadhi hii ni ya tatu kwa ukubwa Tanzania kwa kuwa na eneo la kilomita za mraba 4471.

Pamoja na Hifadhi za Wanyama za jirani za Rukwa, Lukwati na Luafi na misitu ya hifadhi mingi, mfumo ikolojia huu wenye eneo la kilomita za mraba 25,000 ni kitovu cha mojawapo ya maeneo makubwa na yenye hazina kubwa ya wanyamapori na misitu nchini Tanzania. Hifadhi ya Tanzania ya Katavi imepata jina lake kutokana na mzimu wa Katabi(kutoka kabila la Wabende). Hekaya inasema kuwa mzimu huo unaishi karibu ya Ziwa Katavi katika miti pacha (Tamarindus indica na Faidherkia albida). Ziwa Katavi ni ukanda wa mbuga, wakati wa kiangazi na kubadilika kuwa ziwa lenye kina kidogo mwanzoni mwa mvua za masika (Oktoba hadi April). Wastani wa mvua ni takriban milimita 930 na kuwa na misimu miwili ya mvua ambapo mvua fupi huwa Februari.

Mito yote katika Hifadhi ya Taifa ya Katavi isipokuwa mto wa msimu wa Nkanuba uliyopo Kaskazini-Magharibi unatiririsha maji yake kuelekea magharibi kwenye Ziwa Tanganyika, inatiririsha maji Ziwa Rukwa, ni ziwa lenye maji chumvi kiasi lisilo na mto wa kutolea maji (Ziwa la Mwisho). Kusini ni Bonde la Ufa la Rukwa (takriban kilomita 2,300 za mraba).





# Hifadhi ya Mkomazi

## HIFADHI YA MKOMAZI

Hifadhi hii ipo chini ya miteremko ya Safu ya Milima ya Tao la Mashariki inayovutia ya Usambara na Upare yenye nyasi za kijani na kuonekana kwa mbali kutoka kilele cha mlima Kilimanjaro chenye theluji. Mkomazi ni hifadhi isiyoharibiwa inayoonyesha mvuto wa pekee na hazina za kimaumbile na eneo kubwa la wazi- huongeza kutimiza matarajio makubwa ya raha ya mgeni, ni kiungo kinachohitajika sana kati ya vivutio vya ukanda wa Kaskazini na mwambao.

Ipo kaskazini mwa Tanzania katikati ya mpaka wa Kilimanjaro na Tanga, hifadhi hii ina ukubwa wa kilomita za mraba 3,245 (maili za mraba 1,240).

Hifadhi hii inapakana pia na Hifadhi ya Taifa ya Tsavo magharibi nchini Kenya. Mlango wa kuingilia wa Zange upo kilomita 112 (maili 69) kutoka Moshi, kilomita 550 (maili 341) kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu J.K Nyerere- Dar es Salaam;





Kilomita 142 (maili 88.7) kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), kilomita 120 (maili 75) kutoka Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro- paa la Afrika na Kilomita 6 (maili 3.7) kutoka mji wa Same.

## KUFIKA

Kwa barabara, Mkomazi inafikika kwa urahisi kupitia Same, ipo kwenye barabara kuu ya lami inayounganisha Arusha hadi Dar es Salaam.

## MAJIRA

Mwishoni mwa Juni hadi mwanzoni mwa Septemba ndicho kipindi kizuri zaidi cha kuangalia wanyama wakubwa na ndege. Mandhari ya kuvutia zaidi ni Machi hadi Juni.



# Mbunga ya Saanane



## HIFADHI YA SAANANE

Muonekano wa Kisiwa cha Saanane uwapo Mwanza na muonekano wa Ziwa Victoria kutoka katika Kisiwa cha Saanane ni kivutio kikubwa kwa wageni wanaotembelea hifadhi hii.

Hifadhi ya Saanane, ilianzishwa kama bustani ya kwanza ya wanyama nchini mwaka 1964. Lengo la kuanzisha kwake ilikuwa kuhamisha uhifadhi na kuelimisha jamii. Jina la hifadhi hii lilitokana na mwanzilishi wa bustani aliyeitwa Saanane Chawandi.

Kati ya Mwaka 1964 na 1966 wanyama mbalimbali walihamishiwa katika Kisiwa hiki. Wanyama hao baadhi yao ni Mbogo, Digidigi, Tembo, Pofu, Pundamilia, Pongo, Swala pala, Ngiri, Twiga, Nungunungu na Mamba.

Wanyama wakali kama Faru na Mbogo walifungiwa na wanyama wapole waliachwa huru.

Bustani hii iligeuzwa kuwa pori la akiba (game reserve) mwaka 1991. Muonekano wa Ziwa Victoria kutoka katika Kisiwa cha Saanane ni kivutio kikubwa.

Vilevile muonekano wa Kisiwa cha Saanane uwapo jijini Mwanza ni kivutio kingine kikubwa. Hifadhi hii ina eneo la kilomita za mraba 0.5, na iko umbali wa km 2 Kusini Magharibi kutoka katikati ya jiji la Mwanza, katika Ghuba ya Ziwa Victoria.

Kisiwa cha Saanane kinafikika kwa boti ukiwa Mwanza. Mtu anaweza kufika Mwanza kwa gari, ndege ama treni na kutoka Mwanza mjini kutembea kwa miguu ama kwa gari hadi geti la kuingilia hifadhini.

Shughuli za kufanya hifadhini Saanane ni pamoja na kuangalia wanyama, kukwea miamba, kutizama ndege, na safari za kutembea.

Vilevile, kupiga makasia kwa kutumia boti za wenyeji inaruhusiwa kupitia kwa mawakala wa utalii. Hifadhi hii tarajiwa inafikika wakati wowote wa Mwaka.


NMB
Karibu yako
Lango la
Usafirishaji
Kuvuka
Mipaka
MSHIRIKA wa Serikali katika
kujenga TAIFA bora zaidi!
Fanya malipo
ya Serikali
NMB Wakala
Tawi la NMB
NMB Mkononi
Piga *150*66 # au Pakua APP
Download on the App Store
GET IT ON Google Play
www.nmbbank.co.tz

# Hifadhi ya Kilimanjaro

## HIFADHI YA KILIMANJARO

Mlima Kilimanjaro ni miongoni wa vilele virefu vinavyofikika duniani, ni alama kwa wageni wengi kutoka duniani kote ukiwa na kilomita za mraba 1668 (maili za mraba 641), Kaskazini mwa Tanzania, karibu na mji wa Moshi wapandaji mlima wengi wanafika katika ukingo wa Kreta kwa kutumia fimbo ya kutembelea, mavazi yanayofaa na nia thabiti.

Kwa wale wanaofika kilele cha Kibo, ambacho ndicho kilele halisi au kilele cha Gillman kwenye ukingo wa kreta, watapewa hati za kupanda mlima na kumbukumbu zao. Jina lenyewe Kilimanjaro lina maana ya miujiza iliyojificha kwenye mawingu. Lakini pia inaweza kuwa na maana ya Mlima wa Mwanga, Mlima wa Ushujaa au Mlima wa Misafara. Au pengine lisiwe na maana hiyo.

Wenyeji, ambao ni wachaga, nao hata hawana jina la safu yote ya mlima, ni neno kipoo tu (ambalo sasa linajulikana kuwa Kibo) kutokana na kilele maarufu chenye theluji kilichosimama kwa ufahari,

Msimamizi wa bara la Afrika, kilele cha Afrika.

Kilimanjaro, kwa jina lolote liwalo, ni tamathali inayomaanisha uzuri wa Afrika Mashariki unapouona, unaelewa kwa nini.

Mlima huo si kilele kirefu tu cha bara la Afrika, bali ni mlima mrefu zaidi unaosimama pekee duniani, unasimama pekee kutoka kwenye mwambao wenye tambarare yenye vichaka- wenye mwinuko wa mita 900- hadi mita 5,895 za fahari (futi 19,336) Mwinuko wa zaidi ya mita 4,000, jangwa la miti ya misindano halina zaidi ya mimea na nyasi za kijani, kijivu au njano inayoota kwenye ardhi na miamba.



MLIMA KILIMANJARO NI MIONGONI WA VILELE VIREFU VINAVYOFIKIKA DUNIANI, NI ALAMA KWA WAGENI WENGI KUTOKA DUNIANI KOTE UKIWA NA KILOMITA ZA MRABA 1668 (MAILI ZA MRABA 641)



Mwisho kuna mabaki ya uoto ya hapa na pale yenye ardhi ya barafu na theluji- na uzuri wa kuvutia wa paa la bara la Afrika.

**KUFIKA**

Kilomita 128 kutoka Arusha (maili 80). Kiasi cha mwendo wa saa moja kwa gari kutoka uwanja wa ndege wa Kilimanjaro.

**MAJIRA**

Hali ya hewa inayofaa zaidi na yenye joto zaidi ni kuanzia Desemba hadi Februari, lakini pia hali ya ukame (na baridi zaidi) kuanzia Julai hadi Desemba.

**TAHADHARI**

Unapoanza kuupanda mlima huo panda polepole, tumia muda wako mwingi kuzoea hali ya hewa ili kujiongezea uwezekano wa kufika kileleni.


Royal tour
Hifadhi ya
Arusha

## HIFADHI YA ARUSHA

Hifadhi ya Arusha ni hifadhi ya Taifa iliyokaribu zaidi na jiji la Arusha- Mji Mkuu wa safari za kitalii, ulioo Kaskazini mwa Tanzania.

Hifadhi hii ni sawa na kito chenye sura nyingi, ina kilomita za mraba 552 (sawa na maili za mraba 212) na ipo Kaskazini - Mashariki mwa Jiji la Arusha.

Upeo wa hifadhi ni mlima Meru ambao ni mpwa wa mlima Kilimanjaro- ambao ni watano kwa urefu barani Afrika wenye urefu wa mita 4,566 (sawa na futi 14,990).

Vilele vyake na miteremko yake ya mashariki vimehifadhiwa ndani ya hifadhi ya taifa, mlima Meru unaonyesha mandhari yasiyo kifani ya mlima maarufu wa jirani, wakati huo huo unaunda mahali panapopendeza kutembea kwa miguu kwa kujiamini.

Kwanza unapita kwenye pori la Savana, unakokutana na Nyati na Twiga mara kwa mara, unapopanda mlima Meru unakupeleka kwenye msitu unaowaka na kuonyesha mandhari na kudondokewa na majani na nyasi nyororo, kabla ya kufikia nyika ya wazi yenye lobelia kubwa.

Maua ya kudumu yamestawi kwenye jangwa la mlimani na kushikilia kama mimea michanga na kupendezesha matembezi ya kitalii kwa miguu.

Katika pande mbili za kilele chenye majabali, huonekana waziwazi mlima Kilimanjaro, uking'ara rangi ya dhahabu wakati jua linapochomoza.

Mlango wa kuingilia una kivuli cha msitu wa mlimani wenye kima na ndege aina ya  turacos na trogons wa kupendeza- ni mahali pekee katika ukanda wa safari za kitalii ambako Mbega wa rangi nyeupe na nyeusi warukao mitini wanapoonekana kwa urahisi.

Katikati ya msitu inaonekana Ngurdoto Crater, yenye miinuko yake mikali ya majabali inafunika eneo pana la kinamasi lenye Nyati na Ngiri.

Upande wa Kaskazini zaidi, kuna safu ya vilima vyenye nyasi vinavyofunika uzuri uliotulia wa maziwa ya Momela, kila moja lina rangi tofauti ya kijani au bluu.

Wakati mwingine anga lake huonekana rangi ya pinki inayotokana na maelfu ya flamingo, maziwa yana makundi mengi mbalimbali ya ndege wa majini wa kudumu na wanaohamahama, Kuro wenye manyoya yaliyotimka wanaonyesha pembe zao zenye umbo la kinubi pembeni mwa maji.

Twiga wanatembea tembea kwenye vilima vyenye nyasi katikati ya makundi ya Pundamilia wanayokula nyasi, wakati jozi ya digidigi/paa wenye macho makubwa wanaoingia kwa kasi kwenye msitu laini kama Sungura wakubwa wenye miguu mirefu na miyembamba.

## MAJIRA

Kipindi cha kupanda mlima Meru ni Juni- Februari, ingawa mvua inaweza kunyesha mwezi Novemba.

Royal tour



# Hifadhi ya Tarangire

WAKATI WA KIPINDI CHA MASIKA WANYAMA WANAOKUJA KWA MSIMU HUZAGAA KWENYE ENEO LA ZAIDI YA KILOMITA ZA MRABA

**20,000**

Hifadhi ya Taifa ya Tarangire ipo umbali wa kilomita 118 (sawa na maili 75) Kusini- Magharibi ya Arusha, ina ukubwa wa kilomita za mraba 2850 (sawa na maili za mraba 1,096).

Ina mkusanyiko mkubwa wa wanyama nje ya ikolojia ya Serengeti ni mlo wenye vyakula anuwai kwa viumbe wanaokula nyama- na sehemu pekee nchini Tanzania ambapo Mbawala/Paa wa maeneo ya ukame kama vile Choroa mwenye masikio yenye matamvua gerenule wa ajabu mwenye shingo ndefu wanaonekana mara kwa mara.

Mto Tarangire umekauka hadi kwenye kivuli chake cha msimu wa mvua. Hata hivyo kumejazana wanyama.

Wakati wa kipindi cha masika wanyama wanaokuja kwa msimu huzagaa kwenye eneo la zaidi ya kilomita za mraba 20,000 (sawa na maili za mraba 12,500) mpaka wanamaliza uwanda wa kijani na mto kurudi tena.

Lakini makundi ya Tembo wa Tarangire ni rahisi kudhibitiwa, wakati wa mvua au kiangazi.

Maeneo ya Kinamasi yanakuwa ya rangi ya kijani mwaka mzima na kuwavutia zaidi ya aina  za ndege 550, ni eneo linalozaliana spishi nyingi mahali pamoja ambalo hakuna mfano wake duniani.

Chatu wa Tarangire, wanapanda kwenye miti, kama wanavyofanya Simba na Chui wa hapo, hujiegemeza kwenye matawi ambapo matunda ya miti wa soseji huwa kama yanayovutwa na mkia.



# Hifadhi ya ziwa Manyara







INA ENEO LA KILOMITA ZA MRABA

330



## HIFADHI YA ZIWA MANYARA

Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara ipo Kaskazini mwa Tanzania. Mlango wa kuingilia upo umbali wa kilomita 126 savana maili 80, mwendo wa saa 1.5 tu magharibi ya Arusha kwenye barabara mpya ya lami, karibu na soko la wenyeji la Mto wa Mbu.

Ina eneo la kilomita za mraba 330 (sawa na maili za mraba 127), ambapo hadi kilomita za mraba 200 (sawa na maili za mraba 77) ni ziwa wakati viwango vya maji vinapokuwa vikubwa.

Ikienea kwa umbali wa kilomita 50 kwenye kitako cha genge la Bonde la Ufa la rangi ya dhahabu lenye kimo cha mita 600.

Ziwa Manyara ni kito cha kuvutia, lililosifiwa na Ernest Hemingway kama, "lakupendeza zaidi ambalo sijawahi kuliona barani Afrika"

Kuanzia mlango wa kuingilia, barabara inapinda kupitia kwenye eneo pana na la wazi la msitu uliostawi wa chemchem ambapo makundi ya Nyani 100 wenye nguvu wanaishi bila ya papara pembeni mwa barabara, Kima wanakimbia kwa kasi kwenye miti ya mikangazi, Bushbuck nao wanapita kwa hofu kwenye vivuli, Hondohondo wakubwa wa msituni wanalia kwa sauti kubwa mchanganyiko kwenye matawi ya juu ya miti yenye majani yaliyotanda.

Kinyume na ukaribu wa msitu ni eneo la uwanda wa mafuriko wenye nyasi na mandhari pana kuelekea mashariki, kupita ziwa lenye magadi, hadi kwenye vilele vya rangi ya bluu vya volkano vilivyochongoka huchomoza kutoka kwenye Mbuga pana za Wamasai zisizo na ukomo.

Makundi ya nyati wakubwa, nyumbu na pundamilia wanakusanyika kwenye uwanda huu wa nyasi, kama wanavyofanya Twiga, ambao baadhi yao wana rangi ya kiza kiasi kwamba wanaonekana weusi kutoka mbali.

Ndani ya uwanda wa mafuriko, kuna ukanda mwembamba wa mijohoro inayopendwa sana kuwa maskani ya Simba wanaopanda miti na Tembo wenye pembe za kupendeza.

Makundi ya Nguchiro wenye mistari hukimbia kati ya mijohoro, hali ya kuwa digidigi wa kirk wanakula nyasi kwenye vivuli vyao.

Jozi za Wipspringer mara nyingi huonekana wakipiga taswira kwenye miamba juu ya konde linalounguzwa na chemchem ya joto inayotoa mvuke na kububujika ubavuni mwa ufuko wa ziwa upande wa Kusini wa hifadhi.

Manyara ina wingi wa kutosha wa chanzo cha ndege wa Tanzania. Zaidi ya spishi 400 zimerikodiwa. Hata mgeni anayetembelea Afrika kwa mara ya kwanza hatakosa kuona spishi zaidi ya 100 kwa siku. Vivutio vikubwa ni pamoja na maelfu ya Flamingo wenye rangi ya pinki wakiwa katika uhamaji wao wa kudumu, pamoja na ndege wakubwa wengine wa majini kama vile Wari, Cormorants na Korongo.

# Hifadhi ya Mlima Udzungwa



INA UKUBWA WA KILOMITA ZA MRABA 1,990 (MAILI ZA MRABA 770) NA IPO UMBALI WA KILOMITA 350/MAILI 215, SAA 5 KUTOKA DAR ES SALAAM, KILOMITA 65 (MAILI 40) KUSINI – MAGHARIBI MWA MIKUMI.



## HIFADHI YA MILIMA YA UDZUNGWA

Udzungwa ni mfuatano mkubwa na wenye bionuwai nyingi wa milima na misitu inayoinuka kwa madaha kutoka pori tambarare la mwambao wa Mashariki ya Tanzania.

Ina ukubwa wa kilomita za mraba 1,990 (maili za mraba 770) na ipo umbali wa kilomita 350/maili 215, saa 5 kutoka Dar es Salaam, kilomita 65 (maili 40) Kusini – Magharibi mwa Mikumi.

Kwa jumla hujulikana kuwa milima ya Tao la mashariki, mrundikano huu wa milima iliyotengwa inayotajwa pia kuwa ni African Galapagos hutokana na hazina kubwa ya mimea na wanyama vinavyopatikana katika eneo hilo tu, na kujulikana kuwa ni African Violet (iliyorahisi kuharibiwa).

Udzungwa pekee ni miongoni mwa safu ya milima ya kale ya Tao la Mashariki ndiyo iliyopewa hadhi ya hifadhi ya Taifa.

Aidha ni ya kipekee nchini Tanzania kutokana na majani na matawi ya msitu kutanda kuanzia mwinuko wa mita 250 (futi 820) hadi zaidi ya mita 2,000 (futi 6,560) bila kukatizwa.

Si eneo la kawaida la kuangalia wanyama lakini ni kivutio kikubwa cha wanaotembelea mtandao wa kuvutia wa njia za msituni ukijumuisha eneo maarufu la matembezi ya nusu siku hadi Maporomoko ya Maji ya Sanje, yanayotumbukia mita 170 (futi 550) katika manyunyu ya ukungu hadi kwenye bonde lenye misitu chini yake.

Njia ya Mwanihama inayotumia siku mbili inaelekea kwenye uwanda wa juu, na mandhari yake ya kuvutia kwenye mazingira ya shamba la miwa, kabla ya kupanda hadi kilele cha Mwanihama, ambacho ni cha pili kwa urefu katika safu hiyo.

Wataalamu wa elimundege wanavutiwa sana na Udzungwa kutokana na utajiri mkubwa wa ndege wenye aina zaidi ya 400, kuanzia Kiambizi wanaoonekana kwa urahisi wenye kichwa cha kijani, aina zaidi ya aina 12 za ndege wanaojificha kwenye Tao la Mashariki.

Spishi nne za ndege za kipekee za Udzungwa ni pamoja na ndege wa msituni aliegunduliwa kwa mara ya kwanza mwaka 1991 na mwenye asili ya Asia zaidi kuliko ndege mwingine yeyote wa Afrika.

Kati ya mamalia sita wa hali ya juu waliofanyiwa utafiti na kuandikwa, kima mwekundu wa Iringa na Sanje Crested Mangabey ambao hawapatikani kokote duniani – huyu wa mwisho, hasa, hakuwai kubainika na wataalamu wa biolojia kabla ya 1979.

Bila shaka, msitu huu mkubwa na maarufu bado una hazina nyingi za kuvumbua: utafiti wa kisayansi unaoendelea utaongeza anuai zake za viumbe zilizoorodheshwa.







## HIFADHI YA GOMBE

Hifadhi ya Taifa ya mto Gombe ndiyo hifadhi ndogo sana iliyopo umbali wa kilometa 16 (maili 10) kutoka Kaskazini ya Kigoma kwenye ufuko wa ziwa Tanganyika, Magharibi mwa Tanzania, yenye ukubwa wa kilomita za mraba 52 (maili za mraba 20 tu).

Ni eneo nyeti la makazi ya Sokwe mtu wanaoishi kwenye miteremko mikali na mabonde ya mto yanayoelekea kwenye ufuko wa mchanga wa Kaskazini mwa Ziwa Tanganyika.

Kuna Sokwe mtu waliozoeleka kutembelewa na binadamu walipewa umaarufu na kazi ya mtafiti Jane Goodall, ambaye mwaka 1960 alianzisha mpango wa utafiti wa tabia na mwenendo ambao hivi sasa ndiyo utafiti wa muda mrefu zaidi unaoendelea duniani. Mama Fifi, ambaye ndiye pekee aliyebaki kwenye jamii ya awali, wakati Goodall alipowasili mara ya kwanza Gombe, Fifi alikuwa na umri wa miaka mitatu tu, bado anaonekana na wageni.

Sokwe mtu wana kiasi cha 98% ya asili ya binadamu. Hakuhitajiki utaalamu wa kisayansi wa kutofautisha kati ya mkusanyiko wa kutweta kwa pamoja, milio ya kuzomea na upigaji mayowe yanayoonyesha sifa za wakuu, wenye madaraka na za kusaidiana.

Pengine utaona mpepeso wa uelewa unapoangalia macho ya sokwe mtu, na kukutathmini wewe pia, mtazamo wa utambuzi halisi kwenye vipingamizi finyu vya spishi. Mamalia wanaoonekana sana Gombe ni jamii nyingine ya mamalia wa daraja la juu.

Kuna kundi la komba na manyani, wanaofanyiwa utafiti tangu miaka ya 1960; wanatembelewa sana, pia wapo Mbega wenye mikia miekundu na wekundu ambao hili kundi linawindwa sana na Sokwe mtu, Mbega hawa hubaki kwenye matawi ya miti. Kuna spishi zaidi ya 200 za ndege kwenye hifadhi ni pamoja na Tai mla Samaki na wenye mabaka kama ya kito wanaorukaruka kama waliofugwa kwenye kituo cha wageni.


Hifadhi ya
Gombe




## HIFADHI YA KITULO

Wenyeji wanauita Uwanda wa Kitulo kuwa Bustani ya Mungu-wakati wataalamu wa mimea wanauita Serengeti ya Maua, ni wa ulimwengu, maua mengi ya kuvutia.

Ipo Kusini mwa Tanzania kiasi cha kilomita 100 (maili 60) kutoka jiji la Mbeya. Ina eneo la kilomita za mraba 412.9 (maili za mraba 159). Kitulo ni maajabu ya mimea ya tyubu ya spishi 350 ikiwemo aina 45 za maua ya ardhini, yanayojitokeza kama maua ya porini ya aina na ukubwa wa kustaajabisha wakati wa msimu wa mvua mwishoni mwa Novemba hadi Aprili. Ikiwa juu ya mita 2,600 (futi 8,500) kati ya vilele vya Milima ya Kipengere. Poroto na Livingstone, udongo wa volkano wa Kitulo wenye maji ya kutosha una mbuga za nyasi za milimani nyingi na muhimu nchini Tanzania.

Kitulo- ni kivutio cha wataalamu wa mimea na wanaotembea milimani ni kivutio kikubwa cha wanaopenda kuangalia ndege. Ni maskani pekee Tanzania ya makundi ya ndege walio hatarini kutoweka kama vile Denham Bustard, Blue Swallow, Mountain Marsh Widow, Njombe Cisticola wala nafaka wa Kipengere. Aina mbalimbali za vipepeo, vinyonga, mijusi na vyura wanaopatikana, wanaongeza utajiri wa kibiolojia wa Bustani ya Mungu.

## KUFIKA

Kutoka Chimala, kilomita 78 Mashariki ya Mbeya kwenye



IPO KUSINI MWA TANZANIA KIASI CHA KILOMITA 100 (MAILI 60) KUTOKA JIJI LA MBEYA. INA ENEO LA KILOMITA ZA MRABA 412.9 (MAILI ZA MRABA 159).

barabara kuu ya lami iendayo Dar es Salaam, elekea Kusini kwenye barabara ya changarawe inayojulikana kama Hamsini na Saba (57) kutokana na idadi ya kona za umbo la 'U' katika barabara hiyo, hadi maskani ya muda ya hifadhi yaliyopo Matamba, ambapo ni umbali wa safari ya saa moja mpaka kwenye uwanda. Usafiri muhimu na wa mara kwa mara pia upo.

## MAJIRA

Maua ya porini huonekana kwa wingi zaidi kati ya Desemba na Aprili. Miezi ya Kiangazi ya Septemba hadi Novemba inafaa zaidi kwa kutembea milimani ingawa haifai kwa wataalamu wa mimea. Hali ni baridi na ukungu kuanzia Juni hadi Agosti.

## MALAZI

Mbeya ina huduma zote za malazi kuanzia hoteli za starehe hadi nyumba za wageni za kawaida na nyumba mbili za wageni zipo Matamba. Mpaka sasa hakuna huduma za malazi katika hifadhi, lakini malazi muhimu na chakula hupatikana karibu na shamba la Kitulo ndani ya hifadhi kunatarajiwa kuwapo maeneo ya kupiga kambi, yatakayo wahudumia wapiga kambi wenye vifaa kamili. Kwenye ufukwe wa Matema kuna dahalia mbili zenye gharama za wastani zinazoendeshwa na kanisa.

Kamati ya Taarifa za Tovuti Kuu ya Serikali, ilizirekebisha taarifa za hifadhi jhii Oktoba 19,2015.







## HIFADHI YA RUAHA

Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ni sehemu ya mfumo ikolojia wa Rungwa- Kizigo-Muhesi inayochukua zaidi ya kilomita za mraba 45000.

Mwaka 2008 eneo Tengefu la wanyama la Usangu na maeneo chepechepe muhimu mengine katika bonde la Usangu yalijumuishwa kwenye hifadhi na kufanya kuwa hifadhi kubwa nchini Tanzania na Afrika Mashariki yenye eneo la kilomita za mraba 20,226. Jina 'Ruaha' linatokana na neno la Kihehe la "Ruvaha", lenye maana ya 'mto'. Ni miongoni mwa maeneo machache ya ardhi ya pori maarufu ambapo mtu anaweza kuangalia wanyama pamoja na mandhari ya ardhi ya kuvutia. Hifadhi hii ina wingi wa mimea na wanyama kama vile Tandala wakubwa (Tragelaphus Strepsiceros) wasiopatikana katika hifadhi nyingine yoyote ya taifa. Hifadhi inajivunia sana mfumo ikolojia wake usioguswa wala kuvumbuliwa na kufanya safari za kitalii za wageni kuwa za kipekee sana. Mto Ruaha Mkuu kama ilivyo mito mingine kama vile Mwagusi, Jongomero na Mzombe inakuwa kama mhimili wa maisha ya hifadhi.

Wakati wa msimu wa kiangazi, mito hii huwa ni chanzo kikuu cha maji kwa wanyamapori. Kuna chemchem chache za asili zinazokidhi madhumuni hayohayo.

Katika kilele cha kiangazi, Tembo wanapata maji kwenye mito ya mchanga mkavu kwa kutumia miguu yao ya mbele na mikonga. Moporomoko ya maji yaliyobaki katika Mto Ruaha Mkuu pia ni makazi muhimu kwa Viboko, Samaki na Mamba.

# Hifadhi ya maua Ruaha



# Hifadhi ya Mahale







## HIFADHI YA MAHALE

Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Mahale ni maskani ya Sokwe mtu wanaofanyiwa utafiti sana barani Afrika. Msaada wanaotoa wageni kwa njia ya malipo ya ada ya kiingilio kwenye hifadhi, huipa uwezo hifadhi ya kulinda na kuwakinga sokwe mtu hawa na msitu wa kuvutia wanamoishi.

Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Mahale ni maarufu kwa kuwa na baadhi ya Sokwe mtu wa porini wa mwisho waliobaki barani Afrika na ilitangazwa kwenye Gazeti la Serikali mwaka 1985, ina eneo la kilomita za mraba 1,613 na ipo kiasi cha kilomita 128 kusini ya mji wa Kigoma kwenye ufuko wa mashariki mwa Ziwa Tanganyika. Mpaka wa magharibi wa hifadhi unalinda ukanda mpana wa kilomita 1.6 ubavuni mwa maji ya Ziwa Tanganyika.

Sehemu kubwa ya ardhi ina mikunjo mikunjo na milima, na ina safu ya Milima ya Mahale inayoanzia kaskazini- magharibi hadi kusini-mashariki na kukatisha kwenye hifadhi. Kilele kirefu zaidi (mlima Nkungwe) kuna mita 2,462.



# Hifadhi ya Ngorongoro



The Great Migration





## HIFADHI YA NGORONGORO

Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (NCA) lina kiasi cha kilomita za mraba 8,292. Ni miongoni mwa tarafa tatu zinazounda wilaya ya Ngorongoro katika mkoa wa Arusha.

NCA ilianzishwa mwaka 1959 kwa sheria ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro Namba. 413 ya mwaka 1959 kama eneo la matumizi mbali mbali ya ardhi, lililoteuliwa kuhimiza uhifadhi wa maliasili, kulinda maslahi ya wakazi wenyeji wa asili wa NCA, na kukuza utalii.

NCA ni eneo pekee lililolindwa barani Afrika ambapo uhifadhi wa maliasili unawianishwa na maendeleo ya binadamu. Sehemu muhimu za NCA ni pamoja na Kreta ya Ngorongoro, Tambarare za Serengeti zenye spishi za wanyamapori wahamao kiasi cha milioni mbili za mfumo-ikolojia wa Serengeti-Mara (TAWIRI, 2003) na msitu wa vyanzo vya maji; Hifadhi ya Misitu ya Uwanda wa Juu wa Kaskazini (NHFR) inayojulikana kwa Kimasai kuwa ni "Entim Olturot".

Maeneo mengine muhimu yaliyopo kwenye NCA ni ya kiakiolojia na palentolojia ya Bonde la Oldupai na alama za Unyayo wa Binadamu wa kale zilizogunduliwa Alaitole katika eneo la Ngarusi. Kutokana na sifa mahususi na kuishi kwa uelewano kati ya wanyama pori na watu uliokuwepo kwa miaka mingi, NCA ilipewa hadhi ya kuwa Eneo la Urithi wa Binadamu Duniani na kuorodheshwa kuwa miongoni mwa Maeneo Tengefu ya Viumbe hai na mimea ya Kimataifa na Mpango wa Maeneo Tengefu ya Binadamu, Viumbe Hai na Mimea wa UNESCO.



Royal tour

# Hifadhi ya Rubondo







## KISIWA CHA RUBONDO

Kisiwa cha Rubondo kiko kwenye pembe ya Kusini – Magharibi ya Ziwa Viktoria, ambalo ni bahari ya bara inayotandawaa kati ya Tanzania, Uganda na Kenya.

Hifadhi hiyo ya Taifa ina Spishi nyingi za mamalia asilia, Kima, Membe mweusi, na Nguchiro – wanashirikiana makazi na mazingiria yao na spishi mpya zilizoongezwa kama vile Sokwe, Mbega, Tembo na Twiga ambao wote wananufaishwa na kutofikika kwa urahisi kwa Rubondo. Rubondo pia ni hifadhi ya maeneo ya kuzalia samaki.

Asilimia 90 ya kilomita za mraba 457 (maili za mraba 176) za hifadhi ni msitu wenye unyevu nyevu, sehemu iliyobaki ina mbuga ya wazi hadi matutu ya mafunjo/matete ya kando ya ziwa. Mahali ilipo ni: 02’18’08S031’51’62E – kilomita 150 (maili 95) Magharibi ya Mwanza.



# Hifadhi ya Mikumi



NI SEHEMU KUBWA INAYOFIKIKA YA KILOMITA ZA MRABA 75,000(MAILI ZA MRABA 47,000) ZA ENEO LA PORI LINALOSAMBAA UPANDE WA MASHARIKI HADI BAHARI YA HINDI.



## HIFADHI YA MIKUMI

Hifadhi ya Taifa ya Mikumi iko mpaka wa Kaskazini mwa hifadhi kubwa ya wanyama barani Afrika- Hifadhi ya Selous.
Barabara ya lami ya kutoka Dar es Salaam kwenda Iringa inakatika kwenye hifadhi hii.

Ni sehemu kubwa inayofikika ya kilomita za mraba 75,000(maili za mraba 47,000) za eneo la pori linalosambaa upande wa Mashariki hadi Bahari ya Hindi.

Hifadhi ya Mikumi ni ya nne kwa ukubwa nchini Tanzania yenye ukubwa wa kilomita za mraba 3,230 (maili za mraba 1,250); ni sehemu ya mfumo ikolojia kubwa iliyopo katikati ya Hifadhi ya Wanyama ya Selous.

Mahali: Kilomita 283(maili 175) Magharibi ya Dar es Salaam, Kaskazini ya Selous na kwenye barabara inayokwenda Ruaha, Udzungwa hadi Katavi.

Upeo ulio wazi na wanyama wengi wa Uwanda wa Mafuriko wa Mkata, eneo muhimu la Mikumi, linajaribu kulinganishwa mara kwa mara na Tambarare maarufu za Serengeti.

Likiwa limekatishwa na mtandao mzuri wa barabara za kuangalia wanyama, Uwanda wa Mafuriko wa Mkata, pengine ni mahali panapoaminika zaidi nchini Tanzania kwa ajili ya kuangalia Pofu wenye nguvu, ambao ni jamii ya Swala wakubwa zaidi duniani.

Tandala na Palahala nao wanavutia na kufanya maskani kwenye milima yenye misitu ya miombo inayochomoza kwenye mipaka ya hifadhi.

Simba wana randaranda kwenye mbuga- na makundi ya Pundamilia, Swalapala, Nyumbu, na Nyati wanaohama mbugani- kutoka vichuguu vya mchwa vilivyobapa, au wakati mwingine majira ya mvua, kutoka kwenye vitulio vya juu ya miti. Twiga wanakula miti ya mijohoro inayozunguka mto Mkata, kuna vibungi vya vivuli vinavyopendwa na Tembo wa Mikumi.

Zaidi ya spishi 400 za ndege zimerekodiwa wakiwemo ndege wenye rangi ya zambarau kifuani, ndege wenye shingo ya rangi ya njano wenye miguu mirefu na mwewe wakiungana na ndege wahamiaji kutoka Ulaya majira ya mvua.

Viboko ni vivutio vikubwa kwenye mabwawa yaliyopo umbali wa kilomita tano Kaskazini mwa mlango mkuu wa kuingilia na kusaidiwa na aina mbalimbali za ndege maji wanaobadilika.

## KUFIKA

Ipo barabara nzuri ya lami inayounganisha Mikumi kwenda Dar es Salaam kupitia Morogoro kwa wastani wa usafiri wa gari wa saa nne.

Pia wakati wa kiangazi kuna barabara za kuunganishia Udzungwa, Ruaha na Selous.

Ndege za kukodi kutoka Dar es Salaam, Arusha au Selous. Mabasi yanasafiri kutoka Dar es Salaam hadi makao makuu ya hifadhi ambapo gari za kuangalia wanyama zinaweza kuandaliwa.

# Hifadhi ya Serengeti



INA UKUBWA WA KILOMITA ZA MRABA 14,763 (SAWA NA MAILI ZA MRABA

5,700





## HIFADHI YA SERENGETI

Moja ya vivutio vikubwa kwenye hifadhi hii ni Nyumbu milioni moja kila mmoja wakifuata mwenendo ule ule wa kale, na kutimiza dhima yao ya silika katika mzunguko wa maisha usiokwepeka: wakiwa na mhemuko wa wiki tatu za kusafiri na kupandana, mwenye nguvu mpishe, wakati misururu yenye urefu wa kilomita 40 (sawa na maili 25) inapojitosa kwenye mito yenye mamba wengi katika msafara wa kuhama kwa wingi kuelekea kaskazini kila mwaka; kujaza upya spishi katika ongezeko la muda la wanyama linalozalisha zaidi ya ndama 8,000 wa nyumbu kila siku kabla ya kuanza tena msafara wa kila mwaka wa kilomita 1,000 (sawa na maili 600).

Hifadhi hii ni kongwe zaidi na maarufu, pia ni eneo la urithi duniani, na hivi karibuni imetangazwa kuwa maajabu saba ya dunia, ipo umbali wa kilomita 335 (sawa na maili 208) kutoka Arusha, imeenea Kaskazini hadi Kenya na kupakana na Ziwa Viktoria upande wa Magharibi. Ina ukubwa wa kilomita za mraba 14,763 (sawa na maili za mraba 5,700). Serengeti ni maarufu kwa uhamaji wa wanyama wa kila mwaka ambapo wanyama wenye kwato milioni sita wanakanyaga uwanda wa wazi, wakati zaidi ya Pundamilia 200,000 na Swala wa Thomson 300,000 wanajiunga na safari ndefu na ngumu ya nyumbu kutafuta malisho mapya. Hata kama uhamaji huo umetulia, hakuna ubishi kwamba Serengeti ina mandhari ya kuvutia ya kuangalia wanyama barani Afrika, makundi makubwa ya Nyati, vikundi vidogo vya Tembo na Twiga na maelfu kwa maelfu ya Pofu, Topi, Kongoni, Swalapala, na Swala wa Grant. Kuhimili kama ilivyo utazamaji wanyama ni hisia ya ukombozi wa nafsi ambayo ni sifa bainifu ya Uwanda wa Sengereti, unaoenea kwenye Savana inayopigwa na jua hadi katika upeo wa dhahabu unao metameta jua linapokuchwa. Hata hivyo, baada ya mvua kunyesha, eneo hili kubwa la rangi ya dhahabu, linageuzwa kuwa zulia la kijani lililonakshiwa mauapori. Aidha kuna milima yenye miti na vichuguu vya mchwa vilivyochomoza, mito ikiwa na kingo zenye miti ya mitini na mapori ya mijohoro yenye rangi ya njano kutokana na vumbi.

Bila ya kujali umaarufu wa Serengeti, bado inabaki kuwa hifadhi kubwa ambapo unaweza kuwa binadamu pekee kuona, wakati samba anapofikiria kuzingira kwa fahari, bila ya kutetereka kwenye mlo wake unaofuata.

### JINSI YA KUFIKA

Kupanda ndege za kawaida na za kukodi kutoka Arusha, Ziwa Manyara na Mwanza. Kusafiri kwa gari kutoka Arusha, Ziwa Manyara, Tarangire au Ngorongoro Kreta.

### WAKATI MWAFAKA

Katika kipindi cha Desemba hadi Julai Nyumbu huhama, muda mwafaka wa kuangalia wa nyama wanaokula nyama ni Juni- Oktoba.



# *karibu* ZANZIBAR





## KARIBU ZANZIBAR

Zanzibar inafahamika kama visiwa vya marashi vinavyojumuisha Unguja na Pemba. Mbali na hilo lakini pia inatambulika kama eneo zuri na salama la utalii.

Bahati mbaya idadi kubwa ya watu hawafahamu vivutio vilivyopo visiwani humo, fikra zao ni kwamba Zanzibar ina uzuri wa fukwe za bahari tu, visiwa hivi vimebarikiwa vivutio vingi vya asili vinavyoifanya kuwa maarufu zaidi Duniani.

Jarida la TZ&BEYOND linakuorodheshea baadhi ya vivutio hivyo ambavyo ni Mji Mkongwe, Magofu ya kale, nyumba za ibada za zamani,utamaduni wa Mzanzibari, Kisiwa cha changuu, uwepo wa pomboo kizimkazi, maeneo yaliyokuwa wakiishi viongozi waliopita ambayo yana kumbu kumbu ya kutosha pamoja na Msitu wa Jozani.

## MSITU WA JOZANI

Ni umbali wa kilometa 35 kutoka kusini mashariki mwa Unguja hadi kufika katika hifadhi ya msitu wa Jozani ambao hupatikana katika ghuba ya Chwaka, hifadhi hiyo imepakana na vijiji tisa ambavyo ni Pete, kitogani, Ukongoroni, Chwaka,Unguja Ukuu,Charawe, Michamvi na cheju.

# Utalii Zanzibar













Hifadhi ya msitu wa Jozani una vivutio vilivyogawika katika sehemu Tatu , vikiwemo Daraja la Mikoko, sehemu ya wanyama pamoja na msitu.

## DARAJA LA MIKOKO

Daraja la mikoko lipo kati moja ya kivutio ndani ya msitu huo kutokana na urefu wa daraja hilo pamoja na

Miti ya Mikoko ilivyoshonana na kunawiri vizuri katika maji chumvi yalioko chini ya Daraja hilo la mbao.

Kwa umbali ni dakika 40 kwa miguu kuweza kulimaliza daraja hilo ambalo limepambwa na vipepeo aina mbali mbali kama vile Dadanesi na wengine wengi wenye rangi tofauti tofauti za kupendeza kama vile Karasisi ambaye hupatiakana Zanzibar tu.

Royal tour

# Utalii Zanzibar















Mikoko hiyo ipo ya aina tatu : mikoko meupe,mikoko meusi na mikoko mekundu(magando) ambayo ndio inaengeza hadhi ya Daraja hilo kutokana na miti hiyo kuwa na matawi mengi na mizizi yake huchomo juu ya ardhi kwa kiasi kikubwa jambao ambalo huwezi kuwamini kama mizizi waweza hisi nayo ni jumla ya matawi ya miti hiyo.

## MSITU

Msitu huo una miti ya aina mbali mbali kama mitondoo, mivinje , mikaratusi miti mafuta, mikonge, mikangara shamba na mingi mingineyo, ambayo ina urefu wa ajabu na kushonana juu yake jambo ambalo hufanya jua lisionekane katika eneo hilo.

## WANYAMA

Sehemu ya Wanyama ndani ya Msitu huo ndio iliyoibeba umarufu wa msitu huo kwa kupatikana wanyama ambao adimukuonekana katika hifadhi nyingine yoyote duniani.

# Utalii Zanzibar





Wanyama hao kama vile vile chura wa Jozani,Chui wa Zanzibar, Jongoo wa Jozani, Paa nunga na Kima punju (Red Colobus Monkey) ambao wamekuwa vivutio vikubwa vya utali na kuwafanya watu kila kona ya Dunia kufunga safari na kwenda kuvingalia vivutio hivyo Katika Wanyama wote hao, Kimapunju ndio kivutio kikuu cha watalii kutokana na rangi yake ,umbile na tabia yao ya kuishi ujamaa kama Binadamu.

## KIMA PUNJE

Muonekana wa Kima Punju Uso wake ni mweusi una taji la manyoya meupe, rangi ya pinki kwenye midomo na pua na mkia mrefu wenye rangi nyeusi.

Umri wa kuishi wa Kima Punju ni miaka 20 hivyo katika kipindi cha miaka 20 anayoishi duniani anaweza kuzaa watoto saba, ingawa anaweza kuzaa mapacha lakini huwa ni nadra kutokea.

Kima mchanga anapozaliwa anakuwa mweusi lakini rangi yake hubadilika baada ya miezi sita.

## KISIMA CHA MANGAPWANI

Hiki ni kisima cha chini kwa chini (pango) ambalo lina mwanga hafifu, linatajwa kuwepo kwa zaidi ya miaka milioni 1.6. Pango hilo lina pande mbili zilizoenda mbali, upande mmoja unaelekea magharibi na mwengine kusini ambako baada

## Zanzibar

INAFAHAMIKA KAMA VISIWA VYA MARASHI VINAVYOJUMUISHA UNGUJA NA PEMBA. MBALI NA HILO LAKINI PIA INATAMBULIKA KAMA ENEO ZURI NA SALAMA LA UTALII





ya mita 90 za mwinuko kuna mlango wa kutokea juu unaopitika kwa tabu.

Njia zote hizi zina giza, uwapo ndani ya pango hilo huwezi kusikia chochote zaidi ya mlio wa maji na popo. Pango hilo liligunduliwa katika karne ya 19 na kijana mtumwa aliyekuwa akifanya kazi kwenye shamba la Hemed El Harthy wakati akimtafuta mbuzi aliyetumbukia ndani ya pango.

Historia inaeleza kuwa pango hilo ambalo lina kisima cha maji ambacho kina maji ya baridi na safi ambayo hutumiwa na wanakijiji wa Kijiji cha Mangapwani kwa matumizi ya nyumbani, pia lilitumika kuhifadhia watumwa.

### NGOME YA MJERUMANI

Ndani ya Kijiji cha Mangapwani pia kuna ngome ya mjerumani ambayo aliitumia wakati wa vita ya pili ya dunia.

### JUMBA LA BEIT-AL-AJAIB

Jumba hili ni miongoni mwa vitu vya kipekee vinavyopatikana katika visiwa vya Zanzibar, jumba hilo limehifadhi kumbukumbu za historia ndefu kuhusu ubunifu na maendeleo ya Zanzibar.

# SAFARI YA MIAKA 40

**Tangu Januari 1979 VISION PLUS eye clinic imekuwa mstari wa mbele kwa utoaji wa huduma za macho na miwani jijini Dar es Salaam na Zanzibar.**

**Tunayo kukukaribisha katika kituo chetu kipya cha AFYA HOUSE ili kukupa huduma bora kwenye nafasi ya ziada na uungwana.**

**Tungependa kuwashukuru wateja wetu wote kwa kutupa nafasi nzuri kuwahudumia kwa miaka 40.**

**Ni shauku yetu kuwaridhisha na huduma yetu.**
**Wewe ni msukumo wetu mkubwa kwa sisi kufanya kazi nzuri san ana kumbuka, tunakuthamini.**

**Leo tukiwa na maono wazi ya kesho,kuthibitisha kuendelea na kanuni yetu elekezi ya kutoa huduma bora na teknolojia ya hali ya juu ili kukidhi kila mteja.**

*Ahsanteni Sana*

Wako

*Husseinali Datoo (O.D.)*
Mwanzilishi

TUNAMUOMBA Mwenyezi Mungu atuweke salama na atupe afya mzuri. Amina.

VITUO VYETU

AFYA HOUSE | SHOPPERS PLAZA -MIKOCHENI | SAMORA TOWER - SAMORA AVENUE | ZANZIBAR - MLANDEGE

VISION PLUS the eye clinic

VISION PLUS ZANZIBAR

# UZURI WA FUKWE ZA Zanzibar

Limejengwa miaka ya 1880, lipo barabara ya Mizingani karibu na ufukwe wa bahari ya hindi. Lina nguzo 40 zilizojengwa kwa ustadi mkubwa.

## FUKWE

Zanzibar imebarikiwa fukwe nzuri, miongoni mwake ni ufukwe wa Nakupenda, maarufu kama Pwani ya Nakupenda.

Pwani hii ina maji mazuri yaliyopambwa na rangi ya blue pamoja na mchanga safi mweupe. Fukwe nyengine ni Jambiani ambayo ni sehemu nzuri kwenye mwambao wa Bahari ya Hindi, ufukwe mwengine ni ule wa Kendwa, Nungwi, Paje, Matemwe, Uroa , Kiwengwe  na nyengine nyingi.





# ‘RAIS SAMIA TOUR GUIDE NO. 1’


TIB
DEVELOPMENT
BANK
Your Partner for Growth
Chagua Benki ya Maendeleo TIB
Mshirika Wako Katika Maendeleo
Benki inatoa mikopo kwenye:
• Uendelezaji wa miundombinu
• Maendeleo ya Viwanda
• Uchimbaji wa madini
• Mafuta na Gesi
• Huduma
md@tib.co.tz
www.tib.co.tz

Royal tour



# 'RAIS SAMIA TOUR GUIDE NO.1'

Q&A

## NA SAM DIAH
### MDAU WA UTALII NCHINI



Hatua yake hiyo imesaidia utalii wa ndani kuongezeka kwa kasi kubwa, katika kulihalalisha hili jarida la TZ&BEYOND limefanya mahojiano na mdau wa utalii nchini, Sam Diah, ambaye pamoja na mambo mengine ameeleza namna jitihada za Rais Samia, zilivyoleta tija kwenye utalii.

**TZ&BEYOND:** Royal Tour imeleta tija mliyoitarajia?

**SAM DIAH:** Kawaida unapofanya marketing campaign usitegemee kuvuna hapo hapo, inategemea, inaweza ikakuchukua mwaka, miaka miwili mpaka hata miaka mitano kupata mazao ya kile mlichokipanda. Pamoja na ukweli huo, sisi wadau wa utalii tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa juhudi alizozifanya kama kiongozi wa nchi kutoka hadharani na kuwa Tour Guide namba moja, Marketer namba moja wa nchi kuiambia dunia Tanzania iko wapi, Tanzania ina nini na watakaokuja watakutana na nini.

Tukiri wazi kabisa kuwa kumekuwa na mwamko wa kutosha wa watu kuja nchini kutalii n ahata watanzania wenyewe wanatalii.

Serikali imekuja wakati muafaka, sasa tujiandae kuona mapokea ya dunia kupitia kampeni hizi ambazo zimefanywa na Rais wetu.

**TZ&BEYOND:** Kuna dalili za mafanikio makubwa?



**SAM DIAH:** Dalili zipo kubwa, kwa mfano toka Covid ilipoingia Tanzania na dunia nzima, mimi nakaa Arusha ambako ndio kwenye kitovu cha Utalii.

Kabla ya Royal tour ilikuwa ni nadra sana kuona gari la utalii barabarani, ilikuwa ni nadra sana kuwaona wageni wa kutoka nje, wakiwa barabarani wakitembea wakitafuta kahawa, lakini kuanzia Januari mwaka huu hasa Aprili na Mei tumeanza kuona hali ikirejea kawaida, tumeanza kuona baadhi wa wageni wakija, mfano walianza Zanzibar wageni walijaa na wakawa wanakuja huku bara Day trip, wanakwenda Serengeti wanamaliza halafu wanarudi Zanzibar.

**TZ&BEYOND:** Je tumejiandaa vyakutosha kupokea wageni?

**SAM DIAH:** Hilo ni tatizo la miaka mingi, nikikurudisha nyuma tulipokuwa na mkutano wa Sullivan, Arusha ilijaa kabisa na wageni wengine walilala kwenye nyumba za watu, nakumbuka mimi nilipata Black Americans wakalala nyumbani kwangu, ilikuwa ni katika hali ya kirafiki, lakini ilikuwa inaonyesha kwamba kulikuwa na shida ya maeneo ya kuwalaza hata kwenye mbuga zetu huko na kwenye hoteli.





## *Utalii*

TUKIRI WAZI KABISA KUWA KUMEKUWA NA MWAMKO WA KUTOSHA WA WATU KUJA NCHINI KUTALII







Kwahiyo, wakati tunapofanya jitihada za kuuza bidhaa hii ya utalii, ni vizuri kabisa tukaangalia miundo mbinu ya kuwalaza hao wageni kwasababu kuna athari kubwa ukijenga miundo mbinu ya kuwalaza wageni wengi ndani ya Hifadhi, kuna athari za kiikolojia na za mazingira zitatokea.

Tunapaswa kujua kuwa utalii tunauza uzoefu, hakuna kitu unamuuzia mtu anaenda nacho nyumbani, unamuuzia mandhari tu, anaangalia na kuacha hapo.

Unamfanyia huduma kisha anafurahia ama hafurahii. Akifurahia atarudi, kama hakufurahia basi hawezi kurudi tena.

Lakini pia tunapaswa kujua, mtalii anatakiwa kufurahishwa na mahali anakokwenda kuanzia kwenye ndege, anapotua na mpaka siku atakayoondoka.

Akifurahishwa kwa namna hivyo jua huyo atakuwa ni balozi wenu wa kudumu wa utalii, maana atawaeleza ndugu na jamaa zake juu ya kile alichokiona na kufanyiwa.

**TZ&BEYOND**: ATCL imefungua soko la safari za China, vipi upande wenu, mnalitazamaje soko hili?

SAM DIAH: Soko la China tumelitazama na tumeshalijaribu, hatupingani na jitihada za Serikali katika kutafuta masoko, ukienda kwa hesabu za uuzaji China kwa idadi yao wanaweza kuwa soko kubwa na soko zuri kwenye biashara yetu, lakini kwa uzoefu tulionao wachina wengi sio wapenda utalii, wanapenda wakija wakute Shopping malls, wanapenda kuangalia utamaduni na kwa bahati mbaya sana sekta zetu haziko sawa na za wenzetu, nimekwenda China mara kadhaa wenzetu wana utajiri mkubwa sana wa historia na wamewekeza sana katika maeneo hayo na unaweza ukatembea mwezi mzima hujayamaliza hayo maeneo ya kihistoria, sisi hatuna hivyo.

Ni jitihada nzuri kwa hilo soko la Wachina, lakini sasa kuna hiyo hali, jengine ni kwamba masharti ambayo yanakuja na misafara ya wageni kutoka China ni mingi.


VISION PLUS
EYE CLINIC
TUNAPIMA MACHO | MIWANI YA KILA AINA
must de Cartier
TUNAPOKEA KADI ZA STRATEGIS NA NHIF ZA WABUNGE
Huduma ya uhakika
VISION PLUS
ZANZIBAR
AFYA HOUSE OPP CLOUDS RADIO COCA COLA ROAD
TEL: 0778 227 252
ZANZIBAR TUPO MLANDEGE, BOMBAY BAZAAR




Kuna suala la vyakula, kuna tofauti kubwa sana ya vyakula wanavyokula na vile vinavyopatikana huku chini ya ukanda wa Tropical, kwa hivyo ili kukidhi matakwa yao inatakiwa jitihada kubwa zifanyike kutengeneza wapishi na waongoza watalii watakaoweza kuwasiliana nao na kuwahudumia.

**TZ&BEYOND:** Ipo hoja kwamba kuna tozo nyingi kwa watalii, hili nalo likoje?

**SAM DIAH:** Hilo ni kweli, kwa hali halisi na kwa bahati mbaya sana kwa nchi yetu sekta ya utalii imebebeshwa mzigo wa tozo, iko over regulated, kuna vyombo vingi, taasisi nyingi, kanuni nyingi na sheria nyingi zimebebeshwa kichwani kwa mtoto ambaye anaitwa utalii.

Toka nimemaliza elimu yangu ya Chuo Kikuu, nimekuwa kwenye sekta ya Utalii.

Moja ya malalamiko ya mawakala ambayo inatuletea wageni ambao wengi ni familia ni ughali wa gharama kwenye vivutio vya Tanzania.

Kwa bahati mbaya kabisa mamlaka zinazohusika,zimefumba macho ingawa naamini wanaona biashara inaposhuka, wanaona wageni wanapungua, lakini wanashindwa kutafuta namna ya kuweka unafuu kwa sekta ya utalii.

Wanapaswa kuangalia ni namna gani tutaweza kuingiza wageni








wengi, ni kwa namna gani tutaweza kufanya maulizo ambayo wakala mmoja hata awe mdogo kabisa atapa kwa siku. Mfano akipata maulizo 10 angalau waulizaji watano wathibitishe kuja, kwa sasa hali ni tofauti katika maulizo 10 anaweza kupata uthibitisho mmoja tu au asipate kabisa.

Na kilio kikubwa kinakuwa ni ucheleweshwaji tozo.

**TZ&BEYOND:** Unadhani tumechelewa kuutangaza utalii wetu?

**SAM DIAH:** Bahati mbaya sana mfumo wa utawala kwenye serikali na mfumo wa utawala kwa wanaoshikilia ofisi unabadilika badilika sana.

Mabadiliko ya kila mara ya sera na kanuni kwenye utalii yamechangia kurudisha nyuma jitihada za kuutangaza utalii wetu na ndio maana tunaonekana tunachelewa.

Kwa mfano kila baada ya miaka mitano tuna Waziri mpya kwenye Wizara ambaye

*Utalii*

TUKIRI WAZI KABISA KUWA KUMEKUWA NA MWAMKO WA KUTOSHA WA WATU KUJA NCHINI KUTALII N AHATA WATANZANIA WENYEWE WANATALII.



anakuja na maono, ndoto na fikra zake jinsi ya kuipaisha Tanzania. Kwa mfano Tanzania kwa kipindi cha miaka na tano, ishirini sasa tumekuwa na slogan za kuitangaza Tanzania kama Unforgettable Tanzania, Tanzania The Land of Kilimanjaro, Tanzania The Land of Serengeti, Zanzibar, tumekuwa na slogan za namna hiyo, kwahiyo hiyo nayo imechangia kwakua tumejibatiza majina mwengi sana ambayo yameleta wakati sana katika kuitambua Tanzania.

Lingine ambalo naliona ni mbinu ya pamoja ya kuitangaza nchi (coordinated marketing strategy), sasa hivi utakuta Taasisi za Serikali zina mbinu yake, NCAA inayakwake , TANAPA ina yao, TTB ina yake pia pamoja na taasisi nyingine na zote hizi wanafanya kazi ya kuiuza Tanzania. Kwa mfano kila 'tour operator' ana mbinu zake na yeye, sasa hapa utaangalia mgongano mkubwa uliopo wa upekee wa mbinu za kuitangaza nchi (uniqufication of marketing strategy).



*Utalii*

TUKIRI WAZI KABISA KUWA KUMEKUWA NA MWAMKO WA KUTOSHA WA WATU KUJA NCHINI KUTALII N AHATA WATANZANIA WENYEWE



Hatuna mahali ambapo tunasema tuweka nguvu zetu huku aidha ni Marekani au Mashariki ya Kati au wapi. Na naamini kuwa tukiamua na tukiweza kuweka umakini kwenye marketing strategy kati ya Sekta Binafsi na Sekta za Umma najua tutaipaisha Tanzania naona wenzetu ambao wanafanikiwa wamewaweka Sekta Binafsi mbele na Sekta za Umma wakawa kama wawezeshaji.

Naona kuna juhudi zinafanyika za kujaribu kutengeneza hiyo hali inaweza kuwa ndio mwanzo mzuri wa kufanya hilo, nafikiri linaweza kutufikisha mahali ambapo tutaweza kuitangaza Tanzania vizuri na kutumia wataalamu, tusiogope kuwapa nafasi Sekta Binafsi, kutumia wataalamu wa ndani na wa nje na ikiwezekana tuzalishe vijana wetu wengi sana ambao kwenye suala la marketing, Tehama , technology kwasababu njia ya marketing duniani imebadilika, tunahitaji kuendana na wakati na kwa bahati nzuri Tanzania kwa upande wa Technology tumejitahidi, sasa tunatakiwa tufanye mambo kisasa na kikubwa ni kuwa na ushirikiano wa karibu sana katiu ya




TANZANIA
Unforgettable!

Sekta Binafsi na Serikali kwasababu kwanza Sekta Binafsi wamevaa hivyo viatu na ndio wanafanya hizo shughuli kila siku.

Pia kuwe kuna kusikiliza ushauri wa Sekta Binafsi, kwasasa kuna hali ya kudhani kwamba Serikali wanajua zaidi kila kitu. Ni kweli wao wanaweza wakafanya maamuzi lakini tunaamini ushiriki wa Sekta binafsi ukiwa mkubwa itasaidia sana.

Kingine kinachotucheleweshа ni umbali uliopo kati ya watunga sheria na Sekta Binafsi, tunaona kabisa kuna mambo yanatokea, maamuzi yanafanyika lakini tunaaamini kuwa kama watunga sera wangekuwa na uelewa wa ndani kabisa wa kuwa na ushirikishwaji toka mwanzo mpaka mwisho, naamini maamuzi mwengine yasingefanyika.

Tunatamani ndani ya watunga sera kuwe na wataalamu wa Sekta Binafsi ambao wataweza kuelezea kila kitu ili kuwasaidia watunga sera waweze kutoa maamuzi yao ambayo yanaathiri sekta ya utalii.

Lingine ni, hatua ambayo Rais ameichukua baada ya kukabidhiwa madaraka za kuirejesha nchi katika ramani ya dunia, hatua alizozifanya kwa mfano za kuitangaza idadi ya watu wanaoathirika , kuchukua hatua zakuvaa barakoa, kuchukua hatua za chanjo ni hatua ambazo zimeijengea dunia kujiamini kuhusu Tanzania.

Kwamba nchi nyingi zilishaiweka Tanzania Kushoto na utashuhudia mfano mmoja mzuri ambao umetokea juzi baada ya ziara hizi za Rais tumeona Uingereza imeitoa Tanzania kwenye 'Red List', kwa haraka haraka sio kitu kidogo kwenye biashara yetu, tulishangilia sana.

Ni kitu kikubwa kimefanyika na tunashukuru Rais pamoja na wote wanaotusaidia na tunaamini hata kwenye mataifa mengine wataondoa huo uwoga kuhusu Tanzania na ninaamini kwamba hatua zote zinazofanyika za kuhakikisha kwamba tunapunguza hofu ya huu ugonjwa zitaendelea kufanyika kila eneo ili Utalii ufunguke kabisa duniani na tuanze kurudi kwenye hali yetu ya kawaida ya kibiashara.




Royal tour
TANZANIA
Unforgettable



KCB
BANK
Agency Banking
Internet Banking
I-Bank
ATM
Mobile Banking
Mobi
TISS
EFT
TT
E.A Payments
Government Electronics Payments (GEPG)
Let's talk
Internet Banking App
My experience with KCB Bank is that of modern times...




# MATUNDA YA Royal tour

## Forbes, CNN zaipaisha Tanzania

JARIDA maarufu, lenye ushawishi mkubwa duniani, ambalo limekuwa likifuatiliwa na viongozi, wasomi na watu maarufu la Forbes, limeipaisha Tanzania kimataifa.

Jarida hilo ambalo linachapiswa mara nane kwa mwaka likisheheni uchambuzi na upembuzi wa masuala mbalimbali yanayohusu uchumi, siasa, teknolojia, mawasiliano na masuala mengine mtambuka, limeitaja mbuga ya Wanyama ya Serengeti, Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na visiwa vya Zanzibar kama maeneo bora ya kutembelea.

Forbes iliyaorodhesha maeneo hayo kwenye orodha ya maeneo 22 bora duniani yanayofaa kutembelewa.

Hatua hiyo inatajwa kuchangiwa kwa kiasi kikubwa na filamu ya Royal Tour iliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan.



# CNN NAYO YAKUNWA

Chaneli ya Kimataifa ya Cable News Network maarufu kama CCM yenye makao yake makuu Atlanta nchini Marekani na yenyewe imekunwa na hatua ya serikali ya Tanzania chini ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ya kufunga mitambo ya internet itakayorahisisha huduma ya mawasiliano kwenye Mlima Kilimanjaro.

Katika kufurahishwa na hilo CNN imeandika kwenye ukurasa wake wa kijamii kuwa Kilele cha Afrika chapata mtandao wa haraka. Wameielezea hatua hiyo kuwa itasaidia wapanda mlima Kilimanjaro sasa wanaweza kuwasiliana kwa urahisi.


Royal tour




Tunayo Kila sababu ya kumuunga mkono
Rais Samia Suluhu Hassan katika kuutangaza utalii wetu.

Ewe mtanzania jivunie vivutio vya utalii vya Tanzania,
shiriki kuvitembelea na shiriki kuvitangaza.

*Utalii wa Tanzania fahari ya Mtanzania.*

Utalii

# TANZANIA







TANZANIA
Unforgettable!

# ZANZIBAR


Pemba Island
Unguja
Zanzibar
INDIAN OCEAN
Dar es Salaam
TANZANIA
Mafia Island
Unguja
Nungwi
Kigunda
Kidoti
Jongowe
Potowa
Gazija
Mkokotoni
Matemwe
Uyagu
Mwangaseni
Makoba
Donge
Pwani Mchangani
Bumbwini
Kinyasini
Mahonda
Mkataleni
Upenja
Kiwengwa
Mangapwani
Kiwengwa-Pongwe Forest
Selem
Pongwe
Uzini
Chuini
Bububu
Mpapa
Kibweni
Marumbi
Koani
Pingwe
STONE TOWN
Regezo Mwendo
Chwaka Bay
Chwaka
Jendele
Charawe
Dongwe
Ukongoroni
Jozani Chwaka Bay National Park
Bwejuu
Mchamba Wima
Paje
Chumbe Island Coral Park
Kiwani Bay
Kwebona
Pete
Kitogani
Bwelo
Fumba
Jambiani
Zala Park
Uzi
Kijini
Menai Bay Conservation Area
Nganani
Makunduchi
Kufile
Sokoni
Kizimkazi Dimbani
Pemba Island
Konde
Tumbe
Kiuyu
Kwale
Chumbuni
Chanjani
Finya
Wete
Mchangani
Nyale
Chekea
Mzambaraoni
Chwale
Kojani
Bagamoyo
Piki
Kongo
Ziwani
Kangagani
Ole
Gombani
Wesha
Vitongoji
Chake Chake
Laini
Hurumuzi
Chanjamjawiri
Kipapo
Dodo
Ukutini
Mkoani
Mtuhaliwa
Mkanyageni
Kiwani
Kengeja
Kangani
Kichungwani
Kizungu
Jeni
Mafia Island
Bweni
Jimbo
Kirongwe
Mkarangama
Kipingwe
Kilindoni
Utende
Mwera
Kua



Safe travels

by

WORLD TRAVEL & TOURISM COUNCIL

TANZANIA *Unforgettable!*

Royal tour



# BI.HALIMA MAMUYA: RAIS SAMIA ANASTAHILI *Pongezi*

MBUNGE wa zamani wa viti maalum kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambaye pia ni mdau mkubwa wa utalii nchini ameweka wazi kuwa katika watu ambao wanapaswa kupongezwa kwa kuiamsha biashara ya utalii ndani ya muda mfupi ni Rais Samia Suluhu Hassan.

Mwanasiasa huyo alisema kuwa kitendo cha Rais Samia cha kushiriki kwenye filamu ya kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania kwenye filamu ya Royal Tour kimesaidia kupunguza machungu kwa wafanyabiashara wa utalii, ambao walitaabika baada ya kuibuka kwa janga la Corona.

Katika mazungumzo yake na Jarida hili, alisema kamwe haoni haya kumsifia Rais Samia kwani amefanya mambo mengi.

Yafuatayo ni mahojiano kamili kati ya jarida hili na mwanasiasa huyo, ENDELEA.

**TZ&BEYOND:** MAFANIKIO YA ROYAL TOUR YAMEANZA KUONEKANA?

**BI. HALIMA:** Mimi ni mdau wa utalii na nimefanya kazi na Shirika la utalii kwa 13, nimeanza kujihusisha na masuala ya utalii toka mwaka 1980.

Ajira yangu ya kwanza ilikuwa 1980, katika Shirika la Utalii Tanzania. Nimefanya masuala hay ahata nje ya nchi.



MHARIRI WA JARIDA HILI JIMMY KIANGO, AKIFANYA MAHOJIANO NA MHESHIMIWA HALIMA MAMUYA

Royal tour



Nikiri mama amefanya jambo kubwa na la kupongezwa, Royal Tour imekuja wakati mwafaka, tumetoka kwenye Covid na bado tuko kwenye Covid.

Kumbuka Tanzania ilionekana kama nchi ambayo haijali Covid, tulikimbiza watalii wengi, ujio wa Royal Tour nah atua za Rais Samia za kukabiliana na Covid zimesaidia, sasa watalii wanamiminika.

Royal Tour imekuja kwa wakati wake na itatusaidia sana katika kutangaza utalii. Lakini pili, kwa miaka mitano iliyopita tumefanya mabadiliko mengi ya kisera, na kimfumo katika sekta ya utalii bila kujali mbele tunapokwenda, na bila kujali uwekezaji ambayo tuliuweka katika utalii.

Tukabadilisha mifumo mingi, tukabadilisha vilevile utaratibu wa namna ya kupokea mapato yatokanayo na utalii.

Tukiri tu kwa miaka mitano iliyopita utalii wa Tanzania ulilala. Kujenga soko la utalii si kazi ya siku moja, naamini matokeo ya Royal Tour yataonekana zaidi kwenye miaka ijayo.

Hata hivyo matokeo makubwa ya Royal Tour lazima yachanganywe na mambo mengine, kuwe na kampeni imara na endelevu 'vigorous continuous campaign'. Kuna haja pia ya kuboresha miundo mbinu.

Nilipokuwa Shirika la Utalii, Serikali ilibeba jukumu la kutoa waajiriwa wa sekta ya utalii na kuwafundisha wao wenyewe, kwahiyo Serikali ilikuwa inatoa nafasi za watu kwenda kusoma utalii nje ya nchi kwasababu tulikuwa hatuna chuo cha utalii hapa, tulikuwa na chuo kidogo cha Utalii pale Forodhani Hoteli ambacho kilikuwa kinafundisha zaidi mambo ya Hoteli mpaka hatua fulani, hatua ya mameneja walikuwa wanakwenda kusoma Kenya na nchi nyingine.



# BI.HALIMA MAMUYA: RAIS SAMIA ANASTAHILI *Pongezi*

Jukumu kubwa la kuutangaza utalii lilikuwa la Serikali yenyewe, bahati mbaya hilo liliachwa na jambo jema Rais Samia amelibeba tena.

Kwahiyo sisi wadau wa sekta ya utalii tunasema kuwa tuna manufaa makubwa sana kwakua na Rais mwenye kuujua utalii kama Samia Suluhu Hassan.

**TZ&BEYOND:** Je, sasa tunapaswa kuzifungua ofisi zetu za nje?

**BI. HALIMA:** Ndio, lakini hatuwezi kuzifungua kila mahali. Kwa mfano Kenya wanaofisi nadhani tatu tu za utalii nje ya nchi lakini wana ofisi nyingi zaidi za utalii kwasababu wanatumia ubalozi na wanatumia wale Mabalozi wa Heshima wa utalii, ambao na sisi zamani tulikuwa nao, lakini baadae tukafuta, kwahiyo ni kiasi cha sisi wenyewe kupima kwa uwezo wetu kwa sasa tunaweza kufanya nini.

Muhimu ni kuboresha bidhaa yetu ya utalii maana ukitaka mtu aendelee kunywa chai ile ile nyakati zote itafika mahali ataiacha, ni lazima ulete chai bora zaidi ili kuvutia zaidi, hivyo ndivyo utalii unavyotaka, kila siku kuwepo kitu kipya.

**TZ&BEYOND:** Je, tumechelewa kuutangaza utalii wetu?

**BI.HALIMA:** Tumechelewa na kilichotucheleweshа ni mabadiliko ya kila wakati. Unajua hili ni suala ya uchaguzi 'choice'....hivyo ukibaki unasema hali ya uchumi imeharibika kwahiyo funga ofisi zote na mrudi hapa, au msiende kwenye maonyesho yote fungeni, ukisahau kwamba ili uwe na chai ya maziwa, maziwa yananunuliwa na pesa kutoka kwenye utalii, hicho kimetuchelewesha. Kitu kingine ni kwamba wakati tunafanya ubinafsishaji wa Sekta ya Utalii hatukua tumejipanga. Kwa maana wakati hilo linafanyika sisi tungeimarisha uwezo wa sekta binafsi kwenye Utalii ili kuchukua majukumu yale ambayo yalikuwa yanafanywa na Serikali.

Mimi nimekuwa huko kwenye sekta na wakati mwingine hata nilivyokuwa bungeni pale naona, hivi unapitishaje sheria leo kwa mfano yakuongeza tozo halafu unataka ianze kutumika tarehe 1 Julai, haiwezekani, mtalii anapokuja hapa hajanunua jana na wala hanunui leo, mtalii akija hapa anakuwa ameshajiandaa muda mrefu.

**TZ&BEYOND:** Inaonekana Soko la China hatujajiandaa nalo, hili limekaaje?

**BI.HALIMA:** Tulipokwenda China tuliona kua wana shirika la utalii na makao makuu ya hilo shirika yako huko, wao wanahoteli pia, pia wanafanya kazi ya kuelekeza watalii na wote wanatokea kwenye shirika hilo, tulijifunza mengi lakini tuliporudi hatukueleza tuliyojifunza na kuyaona, na hii ni kwasababu kila mtu ana vipaumbele vyake yani ni mpaka siku











upate mtu mwenye kuweka mbele maslahi ya taifa ndipo mambo yatakwenda.

Bado tunaweza kusema kwamba ukilinganisha ofisi ya China na ofisi nyingine utaona kuna mafanikio lakini tunatakiwa kuendelea kujiandaa zaidi na sio soko la China peke yake hata na Korea, tuwe na miundombinu ambayo inakidhi haja ya watalii.

**TZ&BEYOND:** Hali ya Miundombinu yetu ni rafiki kweli kwa watalii?

**BI.HALIMA:** Kitu ambacho sio rafiki hata kidogo ni barabara, na hazitengenezeki na wakati mwingine kutolewa kwa bajeti ambayo haikidhi mahitaji ya ile barabara au hiyo hela haiji na barabara inaendelea kuharibika.

**TZ&BEYOND:** Hatua ya hifadhi kupewa pesa trilioni 1.3 ili kutengeneza miundo mbinu yao wenyewe inaweza kuleta tija?

**BI.HALIMA:** Inaweza kuleta tija, watu wakiwa na vifaa vyao wenyewe na wakapewa fedha zakuendesha vifaa hivyo italeta tija. Sio kukaa mezani na kuangalia tenda ya mtengenezaji wa barabara. Hauhitaji siasa kwenye hizo kazi.


Royal tour
SUB

**TZ&BEYOND:** Bado tuna muda wa kujiandaa kukabiliana na wimbi la watalii?

**BI. HALIMA:** Muda bado upo, nimesikia kwenye vyombo vya habari, Serengeti watajenga Hoteli nyingine ya nyota tano yenye jumla ya vitanda zaidi ya 600 ambayo itakuwa ndani ya hifadhi na itafanywa na kampuni binafsi. Lakini kwa upande mwingine kuhusiana na wawekezaji, kwa Tanzania amani na utulivu tu havitoshi kumvutia mwekezaji bali kuwe na mazingira mazuri pia ya uwekezaji ambapo ni pamoja na tozo na masharti tuliyoyaweka. Tozo tulizonazo ni mzigo kwa mwekezaji na inapunguza hata hiyo idadi ya wageni wanaokuja.

**TZ&BEYOND:** Kwa upande wa tozo, kwa uzoefu wako unailinganisha vipi Tanzania na maeneo mengine?

**BI. HALIMA:** Tofauti ipo, Kenya hawana VAT kwenye tozo zote za utalii, Tanzania tunapaswa kutoa VAT.

Tunapaswa kubadilika, tuwe tunayaangalia mambo kwa undani kabla ya kuyafunga.

Sekta ya Utalii sasa imebadilishwa imekuwa mkono wa jeshi, utalii sio jeshi, jeshi ni vita, tulikosea kulifanya jeshi usu, ndio tulikosea kuliweka, wao wanafikiria zaidi ulinzi kuliko kuita watu. Huwezi kumfanya meneja wa Utalii kuwa jeshi USU, anafanya nini, anashika bunduki wapi hapo!

**TZ&BEYOND:** Kwa kanda ya Kusini pengine ni nini kinapaswa kufanyika?

**BI.HALIMA:** Kuliwahi kuwa na mpango wa kuendeleza utalii kusini, lakini haukuwahi kufanyiwa kazi. Wala hauna haja yakufanya utafiti mpya, huo uliopo ufanyiwe kazi kulingana na mazingira ya sasa kwakua na maeneo yanajulikana.

Nafasi ya Utalii ni nafasi yakusema karibu, na mtu sahihi wa kufaya jambo hilo ni mwanamke. Hivyo kwenye hii Royal Tour unamuona mwanamke (Rais) anakwambia karibu lazima watu waje kwa wingi.

Tuwe tunajindaa vilivyo tayari kwa Maonyesho ya Expo, mapungufu yawe yanafanyiwa kazi.




Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro
ENROLL
TWIGA MILES
AND GET
1,000
AWARD
POINTS
Discover
Book
Journey
TWIGA MILES
Contact Us
www.airtanzania.co.tz
airtanzania_atcl



UJIO WA FILAMU YA ROYAL TOUR ILIYOFANYWA NA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN UMECHANGIA KWA KIASI KIKUBWA KULIHAMASISHA KUNDI KUBWA LA WATALII KUTOKA NCHINI KENYA, KUTEMBELEA VIVUTIO MBALIMBALI VYA UTALII VILIVYOPO TANZANIA.

KUNDI HILO LENYE WATALII ZAIDI YA 80,000 LIMETEMBELEA NCHINI KATIKA KIPINDI CHA MIEZI SABA KUANZIA JANUARI HADI JULAI, 2022, IDADI AMBAYO HAIKUWAHI KUTOKEA KABLA.

OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU (NBS) IMEELEZA KUWA KATIKA KIPI HICHO  JUMLA YA WATALII 86,220 WALITEMBELEA VIVUTIO VYA UTALII VILIVYOPO TANZANIA WAKITOKEA KENYA, AMBAPO KATIKA KIPINDI CHA MWEZI JULAI PEKEE WALIFIKA WATALII 16,654, KUTOKA NCHI HIYO JIRANI, AMBAYO IMEKUWA MSHINDANI MKUBWA WA BIASHARA YA UTALII.

MBALI NA KENYA PIA TANZANIA ILIPOKEA WATALII KUTOKA KATIKA NCHI MBALIMBALI ZA AFRIKA IKIWEMO BURUNDI WATALII 54,577, MALAWI 27,079, UGANDA 21,080 NA AFRIKA KUSINI 20,868.

FILAMU HIYO YA ROYAL TOUR IMETAJWA KUSAIDIA KUONGEZA IDADI YA WATALII KWA ASILIMIA 105.1 KWA KIPINDI CHA JANUARI HADI JULAI 2022 TOFAUTI NA ILIVYOKUWA KWENYE KIPINDI KAMA HICHO MWAKA 2021.

ONGEZEKO HILO LIMEISUKUMA NBS KUZISHAURI TAASISI ZINAZOTOA HUDUMA KWA WATALII KUBORESHWA ZAIDI KWA KUWA UPO UWEZEKANO MKUBWA WA WATALII KUONGEZEKA ZAIDI.

MKURUGENZI WA TAKWIMU ZA KIJAMII WA NBS, DANIEL MASOLWA NDIE ALIYESEMA HAYO ALIPOKUWA ANATOA TAKWIMU ZA WATALII WALIOINGIA NCHINI JANUARI HADI JULAI 2022.

WATALII WALIOTOKA NJE YA NCHI WALIOTEMBELEA VIVUTIO MBALIMBALI VYA UTALII KWA KIPINDI HIKI WAMEONGEZEKA HADI 742,133 IKILINGANISHWA NA 456,266 WALIOINGIA MWAKA 2021IKIWA NI SAWA NA ASILIMIA 62.1.
WATALII WALIOINGIA KWA MWEZI JULAI 2022 PEKEE WALIONGEZEKA HADI KUFIKIA 166,736



# *Watalii* KUTOKA KENYA WAONGEZEKA TANZANIA

IKILINGANISHWA NA 81,307 WALIOINGIA NCHINI MWAKA 2021 SAWA NA ONGEZEKO LA ASILIMIA 105.1.

HII INAMAANISHA IDADI YA WATALII WALIOONGEZEKA KWA MWEZI JULAI 2022 NI MARA MBILI ZAIDI YA WALIOINGIA NCHINI KIPINDI KAMA HICHO MWAKA 2021.

## ...ASILIMIA 30 WAPITIA ZANZIBAR

KATI YA WATALII 742,133 WALIOINGIA KIPINDI HICHO, 222,449 WALIINGIA NCHINI KUPITIA ZANZIBAR, IKIWA NI SAWA NA ASILIMIA 30 YA WATALII WOTE.

## MAREKANI YAONGOZA

KATIKA MWEZI JULAI PEKEE IDADI KUBWA YA WATALII WALIINGIA NCHINI WAKITOKEA MAREKANI AMBAO NI 17,135, UFARANSA 12,634, UINGEREZA 8,586, UJERUMANI 8,015 NA NETHERLAND 5,102.

WATALII KUTOKA NJE YA BARA LA AFRIKA KWA KIPINDI CHA JANUARI HADI JULAI 2022 WALIOINGIA NCHINI WAKITOKEA MAREKANI NI 51,301, UFARANSA 47,403, UJERUMANI 30,817, POLAND 29,004 NA UINGEREZA 28,275.

## WATALII KUTOKA NCHI ZA AFRIKA

KWA BARA LA AFRIKA KWA MWEZI JULAI IDADI KUBWA YA WATALII WALIOINGIA NCHINI NI KUTOKA KENYA 16,654, BURUNDI 7,966, MALAWI 5,113, AFRIKA KUSINI 4,335 NA RWANDA 4,035.

WATALII KUTOKA BARA LA AFRIKA WALIOINGIA NCHINI KATIKA KIPINDI CHA JANUARI HADI JULAI 2022 NI KENYA 86,220, BURUNDI 54,577, MALAWI 27,079, UGANDA 21,080, AFRIKA KUSINI 20,868.

## NI ROYAL TOUR

HATUA HII INATAJWA KUSUKUMWA KWA KIASI KIKUBWA NA UAMUZI WA RAIS  WA TANZANIA SAMIA SULUHU HASSAN WA KUWA MSTARI WA MBELE KATIKA KUVITANGAZA VIVUTIO MBALIMBALI VYA UTALII NCHINI KUPITIA FILAMU YA ROYAL TOUR ALIYOIFANYA KWENYE VIVUTIO MBALIMBALI VYA UTALII.

FILAMU HIYO IMELETA MAPINDUZI MAKUBWA KWENYE SEKTA YA UTALII UKWELI UNAODHIHIRISHWA NA MAKUNDI MAKUBWA YA WATALII WANAOMIMINIKA NCHINI, TOFAUTI NA ILIVYOKUWA HUKO NYUMA.



# MJUE
# Peter Greenberg

Ni mwandishi wa Habari wa Marekani.
Ni Mhariri wa Makala na Habari za Utalii wa kituo cha televisheni cha CBS.

Greenberg anajulikana kama Mhariri wa Makala za Utalii, pia ni mtayarishaji wa vipindi vya televisheni aliyeshinda tuzo ya Emmy.
Umaarufu wake umekuzwa na kipindi cha Royal Tour ambacho hukitengeneza na kukiratibu.

Kipindi cha Royal Tour hurushwa kwenye televisheni ya CBS.
Kipindi hicho huangazia shughuli za kiutalii zinazofanywa na wakuu mbalimbali wa nchi.

Baadhi ya wakuu wan chi wamempa Greenberg ziara binafsi kwenye zao  ili kuandaa filamu ya masuala ya utalii.

Ameshafanya kazi hiyo na viongozi kadhaa duniani wakiwemo Helen Clark wa New Zealand,

Benjamin Netanyahu wa Israel, Abdul II wa Jordan, Alejandro Toledo wa Peru, Felipe Calder'on wa Mexico, Paul kagame wa Rwanda, Mateusz Morawiecki wa Poland na sasa ni Rais Samia Suluhu Hassan wa Tanzania.



*Peter Greenberg*

MHARIRI WA MAKALA NA HABARI ZA UTALII WA KITUO CHA TELEVISHENI CHA CBS.


TANZANIA
Unforgettable!


Royal tour
TANZANIA
Unforgettable!

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

### WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

## MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA (TMDA)

TMDA
Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

## KUHUSU TMDA

*Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ambayo ilikuwa ikijulikana kama Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ni taasisi ya Serikali iliyo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambayo ina jukumu la kulinda afya ya jamii kwa kudhibiti usalama, ubora na ufanisi wa dawa, bidhaa za tumbaku, chanjo, vifaa tiba na vitendanishi.*

*Iliyokuwa TFDA ilibadilishwa jina na kuwa TMDA mnamo tarehe 1 Julai, 2019 kufuatia marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura 219 kupitia Sheria ya Fedha, Na. 8 ya mwaka 2019 ambayo mbali na kubadili jina la Sheria hiyo kuwa Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219, pia ilihamisha majukumu ya kudhibiti ubora na usalama wa chakula na vipodozi kwenda katika Sheria ya Viwango, Sura 130.*

**DIRA** | Kuwa Mamlaka inayoongoza katika kudhibiti usalama, ubora na ufanisi wa dawa, chanjo, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyingine zinazohusiana na afya kwa wote

**DHIMA** | Kulinda afya ya jamii kwa kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa dawa, chanjo, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyingine zinazohusiana na afya.

## MAJUKUMU

1. Kusajili na kutoa vibali vya majengo ya kutengeneza na kuuza dawa, chanjo, bidhaa za tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi
2. Kukagua maeneo ya kutengeneza na kuuza dawa, chanjo, bidhaa za tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi
3. Kukagua shehena za bidhaa za dawa, chanjo tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya forodha na kwenye maghala ya kuhifadhia bidhaa hizi
4. Kutoa vibali vya kuingizia na kusafirisha nje ya nchi bidhaa za dawa, chanjo, tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi
5. Kusajili bidhaa za dawa, chanjo, tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi kabla ya kuruhusiwa kuuzwa katika soko la Tanzania
6. Kudhibiti majaribio ya dawa, chanjo, bidhaa za tumbaku na vifaa tiba na kufuatilia madhara yatokanayo na matumizi ya bidhaa hizi
7. Kudhibiti matangazo ya dawa, chanjo, bidhaa za tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi
8. Kutoa elimu kwa umma

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA),**
**S.L.P 77150, Dar es Salaam au**
**S.L.P 1253 Dodoma**
**Simu: +255 222 450512/450751/452108**
**Simu ya Bure: 0800110084**
**Nukushi: +255 222 450793**
**Barua Pepe: info@tmda.go.tz Tovuti: www.tmda.go.tz**

0800110084 @tmda_tanzania @tmda tanzania www.tmda.go.tz "TMDA Hulinda Afya ya Jamii"

KUTOKA KWA

# Mhariri Mtendaji

## RAIS SAMIA NI KIONGOZI ALIYEKUJA WAKATI SAHIHI

KUNA tofauti kubwa kati ya kiongozi na mtawala, mtawala huwa mwepesi wa kuagiza, kushuritisha na kuamuru.

Mtawala haioni haja ya kuwa mstari wa mbele katika jambo liwe baya au zuri, kwake shani ni kutuma wengine huku yeye akisubiri kusifiwa, kukwezwa na kulakiwa kwa makofi na shangwe hata kama washangiliaji wako katikati ya lindi la maumivu. Kiongozi yeye yuko tofauti, kiongozi huonesha njia, hujiweka mstari wa mbele katika kufanya jambo, hata kama jambo hilo lina hatari na athari.

Si mwepesi wa kukubali kupongezwa, kusifiwa na kulakiwa kwa shangwe zenye maumivu, haoni soni kukiri kosa pale anapokosea na hujisikia fahari pale anapopata watu wa kumuelekeza ama kumkosoa kwa tija. Rais Samia Suluhu Hassan ni kiongozi, tena ni kiongozi mwenye sifa zote stahiki, ni kiongozi kama mama, dada, shangazi, bibi na rais.

Ujio wake ingawa haukutegemewa, lakini naamini Mungu alishaliona hilo na ndio maana hata baada ya kutokea kwa kifo cha mpendwa wetu Hayati Dk. John Magufuli hakukuwa na mizengwe pomoni katika kumkabidhi kiti aliyekuwa Makamu wa Rais (amabye sasa ni Rais Samia). Nayaandika haya si kwa nia ama dhamira ya kumsifia, la hasha! Nayaandika kwa sababu yanasadifu na kuakisi uhalisi.

Rais Samia amekuja kwenye wakati sahihi, wakati ambao nchi ilikuwa inamuhitaji kiongozi mwenye uwezo wa kulea, kubembeleza na hata kufariji, ikumbukwe kuwa Rais ndie mfariji namba moja wa taifa. Katika kipindi ambacho dunia inapambana na janga la Corona, huku kukiwa na maneno lukuki juu ya chanjo ambazo zilikuwa zikitazamwa kuwa na nia ovu kwa waafrika, Rais Samia bila hofu alijitanguliza yeye mwenyewe kuwa wa kwanza kupata chanjo hiyo.

Si jambo rahisi hata kidogo kwa mtu mwenye mamlaka ya urais kuwa na utayari wa kujitoa kafara kwa ajili ya wengi, alikuwa na uwezo wa kutoa amri tu kwamba watu wapigwe chanjo huku yeye akiwa amekaa Ikulu na hakuna ambaye angebisha, lakini hakufanya hivyo. Kama hiyo haitoshi, Rais Samia yeye mwenyewe aliamua kuuacha urais wake Ikulu na kuingia mbugani, msituni na mwituni kutengeneza filamu ya Royal Tour. Rais Samia alifanya hivi kwa makusudi kabisa baada ya kuona hali ilivyo kwenye uchumi wa nchi na mwananchi mmoja mmoja.

Kwa namna hali ilivyokuwa mwaka 2021, Rais angeweza kuamua kulipotezea suala la kuuchachamua utalii na kufanya mambo mengine, lakini bila kutumia fedha za Serikali aliiona haja ya kulisaidia taifa lake.

TZ&BEYOND tunaamini huu ni uzalendo wa hali ya juu, ambao unapaswa kutukumbusha kuwa Rais tuliyenae amekuja kwenye muda na wakati sahihi. Yapo mengi ambayo naweza kumzungumzia Rais Samia ili kuonesha uhalisia wa yeye kuwa kiongozi na si mtawala, lakini itoshe tu kusema mwanamama huyu ni hazina kwa taifa hili.

Matendo, maneno na mwenendo wake unaakisi nia yake njema ya kumlea mtoto Tanzania kwa upendo ili aweze kusimama kwa miguu yake mwenyewe.

Asante Rais Samia kwa kutuletea Royal Tour ambayo sasa matunda yake tunayaona, nchi imefunguka, vyuma vimeanza kuelegea na kazi inaendelea.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU MBARIKI RAIS SAMIA.**



**Jimmy C. Kiango**
**MHARIRI MTENDAJI**

TRA

TANZANIA REVENUE AUTHORITY

ISO 9001: 2008 Certified

VISION PLUS
EYE CLINIC

KCB BANK

Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

CRDB BANK
Tunakusikiliza

NMB

BOARD OF TRUSTEES
NSSF
NATIONAL SOCIAL SECURITY FUND

TIB CORPORATE BANK
Your Partner Bank

TMDA
Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

# SHUKRANI

za dhati kwa WASHIRIKA WETU




# Experience the power of TemboCARD

Shop locally and internationally at over 44 million merchants and 2 million ATMs

VISA

CRDB BANK

The bank that listens